Nipashe
Jumamosi Februari 8, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0580149
The Guardian digital
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710



# Jafo aagiza aliyechoma Qur'an asimamishwe kazi

UKURASA 3




UKURASA 13

# Bunge laibana serikali ubora mfumo wa elimu

**NI** kutoka awali hadi chuo kikuu, lasema uliopo hauendani na ushindani, mabadiliko ya sayansi na teknolojia... *Endelea uk. 2*



Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, John Mongella (mwenye kofia kushoto), akipita katika gati lililojaa maji kuelekea kwenye Kivuko cha MV Tegemezi, katika Kisiwa cha Maisome, wilayani Sengerema jana, kwaajili ya kuelekea katika Kisiwa cha Kaunda, baada ya kukagua miundombinu ya barabara iliyoharibiwa na mvua. Picha ndogo: Mongella akipanda kwenye kivuko. **PICHA: NEEMA EMMANUEL**

## UPASUAJI UBONGO BILA KUFUMUA FUVU WAIVA MOI

UKURASA 3

# Waziri azuia safari za mafunzo makatibu tawala

UKURASA 2

Scan Hapa



Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu
Google Play
App Store

MICHEZO YANGA , RUVU NGOMA NZITO UK. 32

MAONI, KATUNI UK.6

# PM asema Mikoa 18 imeathiriwa na mvua

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa, amesema mvua kubwa inayoendelea kunyesha katika maeneo mbalimbali, mbali na kusababisha vifo, imeathiri barabara 73 na madaraja kwenye mikoa 18 nchini.

Amesema reli ya Tanga hadi Arusha, na Dar es Salaam hadi Mwanza na Kigoma kwa nyakati tofauti nayo ilifungwa kwa muda kutokana na uharibifu wa mvua.

Akizungumza jana bungeni Jijini Dodoma wakati wa kuahirisha Bunge, Majaliwa alisema mvua hiyo iliyoanza Oktoba mwaka jana ikitarajiwa kumalizika mwishoni mwa mwezi huu, imesababisha vifo kwa watu waishio maeneo ya mabondeni, uharibifu wa nyumba, miundombinu ya usafirishaji ikiwamo ya barabara, reli na madaraja.

"Jumla ya barabara 73 na madaraja katika mikoa 18 ziliathirika. Pia, reli za Tanga hadi Arusha na Dar es Salaam hadi Mwanza na Kigoma kwa nyakati tofauti nazo zililazimika kufungwa kwa muda.

"Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali kwa lengo la kuhakikisha kuwa huduma za usafiri na usafirishaji kwa njia ya barabara na reli katika maeneo yaliyoathirika zinarejea haraka," alisema.

Waziri Mkuu alisema serikali inafuatilia kwa karibu taarifa zinazotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa (TMA) ili kuwafahamisha wananchi mwenendo wa hali ya hewa na kutoa tahadhari kupitia vyombo mbalimbali vya habari na mitandao ya kijamii.

Katika hotuba yake, Waziri Mkuu aliwataka wananchi kutumia fursa hiyo kuchukua tahadhari kwa kuhama sehemu za mabondeni na kuzingatia taarifa za utabiri wa hali ya hewa zinazotolewa na TMA.

Majaliwa aliahirisha Bunge hadi Machi 31 mwaka huu litakaporejea tena kwa ajili ya kuendelea na mkutano wa Bunge la Bajeti, ambao utakuwa wa mwisho kwa Bunge la 11.

# Bunge laibana serikali ubora mfumo wa elimu

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

BUNGE limeitaka serikali kupitia upya mfumo mzima wa elimu kuanzia elimu ya awali hadi chuo kikuu ili kukidhi mahitaji ya sasa.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, Peter Serukamba, alitoa rai hiyo jana alipohitimisha hoja ya taarifa ya mwaka ya kamati hiyo.

Alisema lazima Wizara ya Elimu iangalie elimu inayotolewa kama inaendana na ina uwezo wa kupambana na mabadiliko makubwa ya teknolojia.

"Naibu Waziri (William Ole Nasha) anasema wana mpango wa kuhuisha sera ya elimu, tunaomba serikali itafakari umuhimu mkubwa wa kupitia upya mfumo wa elimu.

"Tuje na mfumo ambao kuanzia 'kindergarten' (chekechea) hadi 'university' (chuo kikuu), tuangalie elimu tunayofundisha mitaala, uwekezaji, fedha zinajibu matakwa ya sasa? Kama hatuhangaiki na hilo, tutapata tabu sana huko tuendako," alishauri.

Alifafanua suala la kuboresha elimu lazima kazi ifanywe na shule za umma na binafsi.

Awali, akijibu hoja za wabunge, Naibu Waziri wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, William Ole Nasha, alisema serikali imechukua jitihada mbalimbali kuboresha mfumo wa elimu.

"Kamati imependekeza iundwe tume ya elimu ili kupendekeza namna ya kuboresha elimu, kwa sasa wizara imeanzisha mkakati wa kuhuisha sera ya elimu, tunategemea wabunge na wadau watahusishwa katika zoezi hilo," alisema.

Aliwaomba wabunge kushiriki kikamilifu watoe maoni yao ya namna ya kuboresha elimu.

Alibainisha kuwa kati ya mwaka 2016 hadi sasa, serikali imejenga mabweni 333 na inaendelea kujenga ili kuwasaidia watoto wa kike wasipate shida yoyote kwenye masomo yao.

"Bajeti ya sekta ya elimu ni halisia na imejikita kwenye mahitaji halisi ya Watanzania, bajeti za huko nyuma zilikuwa zimejaa makokoro mengi na kulikuwa na fedha za kusafiri ovyo nje, fedha za chai ambazo zilikuwa hazisaidii chochote na upigaji mwingine,"alisema.



Magari yakiwa yamenasa katika tope, eneo la Kiangara, katika barabara ya Liwale - Nachingwea, mkoani Lindi juzi, kufuatia mvua zinazoendelea kunyesha maeneo mbalimbali nchini, ambazo zimesababisha maafa na uharibifu wa miundombinu ya barabara: **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Serikali yazuia safari za mafunzo makatibu tawala

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

OFISI ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), imezuia utoaji wa vibali kwa viongozi na watendaji wa mikoa na wilaya wanaoomba kwenda safari zisizo na tija nje na ndani ya nchi.

Pia, imefuta kibali cha makatibu tawala waliokuwa wameomba kuhudhuria mafunzo katika Chuo cha Diplomasia jijini Dar es Salaam mwezi huu.

Hatua hiyo ilitangazwa jana na Waziri Selemani Jafo alipozungumza na waandishi wa habari jijini hapa. Alisema uamuzi huo umetokana na baadhi ya viongozi kutaka kusafiri mara kwa mara nje ya utaratibu, huku wengine wakiomba kwenda nje ya vituo vyao kwa ajili ya semina.

"Tumeshatoa maelekezo kwa barua Agosti 2019 ya kuwaelekeza viongozi wote, wakuu wa mikoa, wilaya, makatibu tawala wa mikoa na wilaya, wakurugenzi wa halmashauri wote wabaki kwenye vituo vyao vya kazi kipindi hiki tunaposhughulika na ujenzi wa miradi ya maendeleo," alisema.

Alieleza kuwa suala la semina na makongamano yasiyokuwa na tija na hayana maslahi kwa wananchi, halikubaliki.

"Naona hii tabia bado inaendelea hapa na pale, nimeona nitoe maelekezo kwamba hata wale waliopata kibali cha kwenda kuhudhuria mafunzo katika Chuo cha Diplomasia jijini Dar es Salaam Februari mwaka huu, namwagiza Katibu Mkuu Tamisemi, Joseph Nyamhanga, kufuta vibali vyote," aliagiza.

Jafo alisema amezuia kuhudhuria mafunzo hayo kwa sasa kwa sababu kuna Watanzania wengi wapo kwenye majanga yaliyotokana na mvua.

"Kuna mafuriko huko yametokea, tunahitaji viongozi wakae washughulikie matatizo ya wananchi, sitarajii kuona kipindi hiki viongozi wanaenda kwenye mambo yasiyo na tija badala ya kushughulika na matatizo ya wananchi," alikemea.

HABARI KITAIFA

## Upasuaji ubongo bila ya kufumua fuvu waja MOI

**Na Mary Geofrey**

TAASISI ya Tiba ya Mifupa (MOI), inatarajia kuanza kutoa huduma za upasuaji wa ubongo bila kufungua fuvu la kichwa (Angio Suite) hivi karibuni baada ya mitambo ya kisasa kuwasili nchini.

Katika taarifa iliyotolewa jana jijini Dar es Salaam na Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano MOI, Patrick Mvungi, ilielezwa kuwa mitambo hiyo iliwasili juzi katika Bandari ya Dar es Salaam na inatarajiwa kusimikwa hivi karibuni.

Mvungi alisema kuwapo kwa mitambo hiyo kutaifanya MOI kuanza kutoa huduma za upasuaji wa matatizo ya mishipa ya damu kichwani bila kufungua fuvu la kichwa.

Alisema serikali ilitoa Sh. bilioni 7.9 kwa ajili ya kujenga maabara ya kisasa ya upasuaji wa ubongo pamoja na ununuzi wa mashine hizo zenye uwezo wa kutibu damu iliyoganda kwenye mishipa ya damu miguuni.

Mvungi alisema ujio wa mitambo hiyo ya upasuaji wa ubongo bila kufungua fuvu utakuwa msaada wa kupunguza rufani za nje ya nchi na kuhudumia nchi jirani za Afrika.

"Mwezi Mei mwaka jana, serikali ilitoa Sh. bilioni 7.9 ili kujenga maabara ya kisasa, itakayosaidia upasuaji wa mishipa ya damu katika ubongo.

"Kwa sasa tunafanya upasuaji kwa kufungua ubongo lakini kuanzia mwezi huu tunaanza kufunga mashine hizi za kisasa na kutoa huduma hii kwa njia ya kisasa," alisema.

Aliongeza kuwa taasisi hiyo pia inatoa huduma mbalimbali za kibingwa na kibobezi zikiwamo; upasuaji wa kuondoa vivimbe vya mishipa ya damu kwenye ubongo na upasuaji wa mgongo kwa kufungua eneo dogo.

Alisema pia zipo huduma za upasuaji wa magoti kwa njia ya matundu, upasuaji wa kupandikiza nyonga bandia, upasuaji wa kupandikiza goti bandia na upasuaji wa kuondoa uvimbe kwenye ubongo.

Alisema kwa sasa huduma hizo na nyingine zinapatika nchini kufuatia maboresho katika sekta ya afya tofauti na awali zilikuwa zinapatikana nje ya nchi kwa gharama kubwa.



Mkurugenzi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), Dk Wilson Mahera, akizungumza wakati wa mkutano na wadau wa uchaguzi, jijini Dar es Salaam jana, kuhusu uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapigakura, linalotarajiwa kufanyika kwa muda wa siku saba katika mikoa ya Dar na Pwani. PICHA: JUMANNE JUMA

# Waziri aagiza aliyechoma Qur'an asimamishwe kazi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, ameagiza kusimamishwa kazi kwa mtumishi wa Halmashauri ya Kilosa mkoani Morogoro, Daniel Elimringi, aliyedaiwa kuchana kitabu cha dini.

Jafo ametoa kauli hiyo baada ya kusambaa kwa picha katika mitandao mbalimbali ya kijamii zikionyesha picha inayodaiwa ya mtumishi huyo wa Halmsahauri ya Kilosa akichana Qur'an.

Akizungumza na waandishi wa habari jana ofisini kwake jijini Ddooma, Jafo alisema ameamua kutoa maagizo kwa Mkurugenzi wa Halmashauli hiyo, kumsimamisha kazi mtumishi huyo na hatua nyingine zichuliwe dhidi yake.

"Nayasema haya kutoka na kuwa mimi ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tamisemi na huyu mtumishi yupo katika wizara yangu kwani Halmashauri ya Kilosa ni moja ya eneo langu, hivyo natoa maagizo haya na yatekelezwe mara moja," aliagiza.

Alisema kitendo kinachodaiwa kufanywa na mtumishi huyo, hakipaswi kufumbiwa macho, hivyo Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Kilosa anatakiwa kuchukua hatua mara moja kumsimamisha kazi.

Pia, alisema mara baada ya kusimamishwa kazi, mamlaka ya nidhamu ichukue nafasi yake katika kuchunguza suala hilo na baada ya kujiridhisha hatua kali zichukuliwe dhidi ya mtumishi huyo.

Vilevile, alimwagiza Mkuu wa Mkoa wa Morogoro na Mkuu wa Wilaya ya Kilosa, kusimamia suala hilo na kuendelea kulinda amani na utulivu uliopo nchini.

"Jambo hili lililofanywa na mtumishi huyu halileti kabisa afya kwa taifa letu kwani watu wake wa dini zote wamekuwa wakiishi katika mazingira ya amani na kuheshimiana kwa kila mtu," alisema.


Maternity Africa
Making childbirth safe

Kivulini, Arusha, Tanzania
info@maternityafrica.org
P.O Box 16464
+255716913934

TAARIFA KWA UMMA

Hii ni taarifa kwa umma kwa ujumla kwamba mtu anayetambulika kwa majina tajwa sio mfanyakazi tena wa **Maternity** Africa kuanzia tarehe **04/02/2020** kwa hivyo haruhusiwi kuwakilisha, kufanya mawasiliano au shughuli yoyote kwa niaba ya Maternity Africa. Dhima yoyote itakayosababishwa na yeye haitatambuliwa.



**Lucas Kuyaya Toroya**

215620602

BEST GROUP (T) LIMITED
Debts collectors, Auctioneer, Commission Agent & Legal Consultant

TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Kwa idhini tuliyopewa na **First National Bank t(FNB),** tutauza kwa mnada wa hadhara dhamana ya wadaiwa wao, ambazo ni Nyumba kama zilivyoorodheshwa kwenye jedwali hapo chini. Mnada utafanyika kuanzia saa **4:00 asubuhi na kuendelea.**

| NA | JINA LA MDAIWA | DHAMANA/MAHALI ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|
| 1. | ANTHONY NESTORY MDULA | Nyumba ya makazi yenye Hati na.41609,LR Mwanza L.O.No.403104 Kiwanja na.904 Kitalu 2, iliyopo eneo la North Buswelu, katika Jiji la Mwanza kwa jina la **ANTHON NESTORY MDULA** | 23/2/2020 |
| 2 | YUSUPH SWALEHE BANYANGA | Nyumba ya makazi yenye Hati na.39143 LR,Mwanza, Kiwanja na.201&202 Kitalu "C", iliyopo eneo la Nyegezi jijijni Mwanza kwa jina la **YUSUPH SWALEHE BANYANGA** | 22 /2/2020 |
| 3 | DIOMEDES R RUTABANZIBWA | Nyumba ya makazi yenye Hati na.18200,LR Mwanza Kiwanja na.192,L.O.No.238623 Kitalu "C" iliyopo eneo la Nyasaka jijini Mwanza kwa jina la **DIOMEDES R RUTABANZIBWA** | 23/2/2020 |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Dhamana itauzwa kama ilivyo.
2 .Mnunuzi atatakiwa kulipa siku ya mnada asilimia 25% ya bei iliyofikiwa.
3. Malipo ya asilimia 75% yalipwe ndani ya siku kumi na nne (14). Kukamilisha malipo yote. Kushindwa kufanya hiyo mnunuzi atakuwa amepoteza malipo yote ya awali ya asilimia 25%, na mnada kurudiwa Au kuchukua mshindi wa pili.
4. Gharama za kuona, kukagua, kuhamisha umiliki, kumtoa mdaiwa/mpangaji na zingine zinazoambatana na hilo ni jukumu la mnunuzi.

Kwa Taarifa zaidi wasiliana na:
Mkurugenzi Mtendaji
Best Group (T) LTD
Alli Hassan Mwinyi Road
Green Acres Buliding, 2nd Floor.
P.O. BOX 1088
DAR ES SALAAM
Contact: +255 715-363537/ +255 765-363537

AU

Mkurugenzi Mtendaji
First National Bank Tanzania Limited (FNB)
Ohio street
P.O.BOX 72290,
DAR ES SALAAM
Contact I:+255 713963596
0758502628
Email: info@fnb.co.tz

215621802

## HABARI KITAIFA

# Ajali ya basi, lori yajeruhi 10

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WATU 10 wamejeruhiwa na wengine kadhaa kunusurika mkoani Mbeya baada ya basi la Kampuni ya Premier lenye namba za usajili T 629 AET, linalofanya safari zake kati ya Jiji la Mbeya na Mwanza, kugongana uso kwa uso na lori lenye namba za usajili T 486 ANU lililokuwa likivuta tela lenye namba za usajili T 775 APT.

Ajali hiyo ilitokea jana asubuhi katika Kijiji cha Darajani, Kata ya Inyala wilayani Mbeya wakati basi hilo likitoka Mbeya kwenda Mwanza, huku lori lililohusika kwenye ajali hiyo likitokea jijini Dar es Salaam kwenda nchi jirani ya Zambia.

Baadhi ya mashuhuda wa ajali hiyo walidai ajali hiyo ilitokea baada ya lori kujaribu kulipita lori lingine lililokuwa limeegeshwa barabarani na ndipo likakutana uso kwa uso na basi hilo lililokuwa likifukuzana na mabasi mengine.

Mzee Herman Kalla wa kijiji hicho, alidai aliliona lori likiyapita magari mawili yaliyokuwa yameharibika na kuegeshwa barabarani, na kabla halijamaliza kulipita gari la mwisho, lilikuja basi la Premeir

INAENDELEA UK. 8




Mkurugenzi Mtendaji wa Foundation for Civil Society (FCS), Francis Kiwanga, akifugua mkutano kuhusu nafasi za Asasi za kiraia kuelekea uchaguzi mkuu nchini, jijini Dar es Salaam jana. Kushoto ni Mwendesha mjadala, Lulu Urio. **PICHA: MIRAJI MSALA**


**Land Form No. 54 A**

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**

**THE LAND ACT, 1999**
(No. 4 of 1999)
**DEFAULT NOTICE**
(Under Section 127)

**Title No 159791, Plot No 757,**
**LO No.696671, Block 'C',**
**Dar Es Salaam**
**Kinondoni, Municipality,**

**To: Francis Bernard Sukari**
**P.O.Box 75479,**
**Dar Es Salaam,**
**0754307445**

That be notified of the default to honour your obligations, covenanted under the mortgage with Maendeleo Bank PLC, whereby you guaranteed **Mwashi Kija Sinas** (Borrower) who failed to repay the loan facilities on due dates to the extent that, as of 07th February, 2020 the outstanding balance was **Tshs 129,826,186.01**

You are hereby required to pay the said **Tshs. 129,826,186.01** so as to rectify the said default. Please be informed that penalties and interest accrues daily.

Be further notified in the event you do not rectify the default stated above within Sixty (60) days from receipt of this notice, we may exercise our right to sell the mortgaged property/land cited above, or appoint a receiver or lease the property, or enter possession or sue you in court.

Dated at Dar es Salaam this 07th day February of 2020.

**FOR MAENDELEO BANK PLC**

..............................................

**Signature of Borrower/Guarantor.**

**Cc. Mwashi Kija Sinas**

MAENDELEO BANK PLC.
P.O. Box 216, DAR ES SALAAM
07 FEB 2020
BRANCH MANAGER
KARIAKOO BRANCH


# Sheria kutatua mgogoro nje ya mahakama yaiva

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

BUNGE limepitisha Muswada mpya wa Sheria ya Usuluhishi ya Mwaka 2020, ambao pamoja na mambo mengine itatumika sasa katika utatuzi wa migogoro ya kimataifa kwa njia ya kirafiki nje ya mfumo wa mahakama.

Sheria hiyo inakusudia kutatua matatizo mbalimbali yaliyokuwa yanaikabili serikali katika kusimamia na kushughulikia masuala mbalimbali yanayotokana na mashauri ya usuluhishi.

Jana, Bunge lilipitisha muswada huo unaopendekeza kufuta Sheria ya Usuluhishi Sura ya 15 na kutunga Sheria mpya ya Usuluhishi ya Mwaka 2020.

Waziri wa Katiba na Sheria, Dk. Augustine Mahiga, wakati anawasilisha bungeni muswada huo, alisema utaruhusu pia kuanzishwa kwa kituo cha kimataifa cha usuluhishi ambacho kitashughulikia usuluhishi wa migogoro ndani na nje ya nchi.

Vilevile, alisema muswada huo unaweka masharti kwa kituo cha usuluhishi kuwa na uwezo wa kujifungamanisha na vituo vingine vya kimataifa vya usuluhishi.

Alisema muswada huo pia unaruhusu sasa kufanyika kwa marekebisho ya Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Madai, Sura ya 33, Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Jinai, Sura ya 20, Sheria ya Mamlaka ya Nchi katika Usimamizi wa Maliasilia, Sura ya 449 na Sheria ya Ubia wa Sekta ya Umma na Sekta Binafsi.

Kwa mujibu wa Balozi Mahiga, muswada huo pia unalenga kuweka utaratibu wa utekelezaji wa mikataba ya kimataifa ya usuluhishi ambayo Tanzania imeridhia, na kuweka mfumo na masharti madhubuti na rafiki katika usimamizi na uratibu wa utatuzi wa migogoro kwa njia ya usuluhishi nje ya mfumo wa mahakama.

"Marekebisho katika sehemu hii yanakusudia kuimarisha mfumo wa utatuzi wa migogoro kwa kupanua wigo wa dhana ya ufifishaji wa makosa ya jinai na kuboresha mfumo wa utatuzi wa migogoro nje ya mahakama kwa kuziwekea utaratibu wa kisheria njia za utatuzi wa migogoro za upatanishi, maridhiano na majadiliano," alifafanua.

Balozi Mahiga alilieleza Bunge kuwa malengo mahsusi katika marekebisho ya Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Jinai ni kupanua wigo wa kifungu cha 163, ambacho kinaruhusu utatuzi wa migogoro kijinai katika jamii kwa njia ya maridhiano pale ambapo mlalamikaji ameridhia kusuluhishwa na mahakama au mtu mwingine anayeweza kuzipatanisha pande zinazohusika katika shauri husika.

Kuhusu mapendekezo ya marekebisho ya sheria zinazohusu ubia baina ya sekta ya umma na sekta binafsi pamoja na ile mamlaka ya nchi na usimamizi wa maliasili za nchi, Balozi Mahiga alisema yanalenga kuwezesha migorogoro inayohusu mali asilia za nchi 22, kutatuliwa kupitia vyombo vya usuluhishi vilivyoanzishwa kwa mujibu wa sheria za Tanzania.

## HABARI KITAIFA

# Kaya 4,000 zanufaika Tasaf Kibaha

**Na Elizabeth Zaya**

MFUKO wa Maendeleo ya Jamii(Tasaf) katika Halmashauri ya Kibaha mkoani Pwani, umefanikiwa kuboresha maisha kwa kaya zaidi ya 4,000 kuanzia mwaka 2014 hadi Februari mwaka huu.

Mratibu wa Tasaf katika halmashauri hiyo, Sijaona Muhunzi, alisema awali zilikuwa zinashindwa kumudu kujigharimia huduma za chakula hata mlo mmoja kwa siku.

Alisema tangu kuingizwa katika mpango, maisha ya wananchi wa kaya hizo yamekuwa bora na umewasaidia kuondokana na matatizo mbalimbali yaliyokuwa yanawakabili.

"Mbali na Tasaf kuwapatia fedha, lakini pia umewasaidia kupata elimu ya ujasiriamali, wapo ambao kwa sasa wanafuga, wanaolima na wamejiunga katika vikundi vyao vya kujiwekea akiba," alisema.

Mtendaji wa Kijiji cha Vikuge ambacho ni miongoni mwa vijiji 45 vilivyonufaika na mpango huo katika halmashauri hiyo, Maximillian Mutobu, alisema walengwa hao wamenufaika kupitia ajira za muda za miradi mbalimbali ya Tasaf ikiwamo ukarabati wa barabara za mitaa.

Vilevile, alisema walipata ajira za muda kupitia uchimbaji wa mabwawa ambayo ujira waliolipwa katika kazi hizo umechangia kuanzisha miradi mbalimbali ya kujiongezea kipato pamoja na kujiwekea akiba.

"Tunaishukuru sana Tasaf kwa kuendelea kusaidia hizi kaya masikini, kabla ya kufika kwa mpango huu hali ya maisha kwa baadhi ya wananchi wetu ilikuwa mbaya sana, lakini mpaka sasa tangu waingizwe kwenye mpango, tumeona mafanikio makubwa.

"Pia, kupitia semina mbalimbali ambazo walikuwa wakipewa, zimewasaidia sana hata kufahamu namna ya kujiwekea akiba hususani katika pesa wanazopata kupitia shughuli ndogondogo za ujasiriamali wanazofanya," alisifu.



Mratibu wa Dawati la Jinsia na Watoto kutoka makao makuu ya Jeshi la Polisi, SSP Faidha Suleiman (kulia) na wadau wengine wa kupinga ukeketaji, wakifuatilia kongamano la maadhimisho ya Siku ya Kupinga Ukeketaji Duniani, lililoandaliwa na Umoja wa Ulaya (EU), jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: SABATO KASIKA**

# NEC yaongeza vituo vya kuandikisha wapigakura

**Na Beatrice Shayo**

TUME ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) imesema uboreshaji wa daftari la kudumu la wapigakura kwa mikoa ya Dar es Salaam na Pwani, utaanza rasmi Februari 14 hadi 20 mwaka huu.

Vilevile, imesema vituo vya kuandikisha wapigakura kwa nchi nzima vimeongezeka kutoka 36,549 hadi kufikia 37,407.

Hayo yalisemwa jana jijini Dar es Salaam na Mwenyekiti wa NEC, Jaji Semistocles Kaijage, wakati wa mkutano wa tume hiyo na wadau mbalimbali wa uchaguzi wakiwamo wanasiasa, viongozi wa dini na asasi za kiraia.

Alisema tayari tume imekamilisha uboreshaji wa daftari hilo katika mikoa mingine ya Tanzania isipokuwa Morogoro kwenye baadhi ya halmashauri na Dar es Salaam na Pwani.

Alisema maandalizi kwa ajili ya uboreshaji wa daftari hilo katika kundi la mikoa ya Dar es Salaam na Pwani yamekamilika na Februari 14 hadi 20 utaanza rasmi.

"Tunaamini mafanikio ya uboreshaji yanategemea ushirikiano wa wadau mbalimbali wa uchaguzi, tume inatambua kuwa viongozi wa vyama vya siasa, viongozi wa dini, wawakilishi wa asasi za kiraia, makundi maalum ya watu wenye ulemavu, vijana, wanawake, wanahabari na wazee wa kimila mnayo nafasi kubwa katika kuleta mabadiliko chanya na mwamko wa kimaendeleo katika jamii zetu," alisema.

Jaji Kaijage alisema uhakiki wa vituo vya kuandikisha wapigakura nchi nzima ulifanyika mwaka 2018 likiwa na lengo la kuona kama vituo hivyo bado vipo na kama bado vina sifa na hadhi ya kuwa vituo vya kuandikisha wapigakura kwa mujibu wa sheria na kanuni za uchaguzi.

Alisema kutokana na uhakiki huo, vituo vya kuandikisha wapigakura kwa nchi nzima viliongezeka kutoka vituo 36,549 hadi kufikia vituo 37,407.

"Kwa Mkoa wa Dar es Salaam, vituo hivyo viliongezeka kutoka vituo 1,614 vya kuandikisha wapigakura vilivyokuwapo mwaka 2015 hadi kufikia vituo 1,661 mwaka 2020, kwa hiyo ni vituo 47 tu vilivyoongezeka katika mkoa huu wa Dar es Salaam," alisema.

Alisema kabla tume haijaanza kutekeleza uboreshaji wa daftari hilo, walifanya maandalizi kadhaa ikiwa ni uhakika wa vituo vya kujiandikisha, uandikishaji wa majaribio, maandalizi ya vifaa vya uboreshaji na kuandaa mkakati wa elimu ya mpigakura.

Alisema uboreshaji huo hauhusishi wapigakura wote walioandikishwa kwenye daftari la kudumu la wapigakura mwaka 2015 bali unawahusu wapigakura wapya ambao wametimiza umri wa miaka 18 na wale ambao watatimiza umri huo siku ya uchaguzi mkuu mwaka huu.

"Uboreshaji huo pia utahusisha wale ambao wamehama kutoka maeneo yao ya awali na kuhamia maeneo mengine, wale ambao kadi zao zimeharibika au kupotea na wale ambao wanatakiwa kuondolewa kwenye daftari kama vile waliofariki dunia au waliopoteza sifa," alifafanua.

Mkurugenzi wa Idara ya Habari na Elimu ya MpiraKura wa NEC, Giveness Aswile, alisema wamekutana na wadau mbalimbali kwa lengo la kuwagusa wananchi kupitia makundi hayo ambayo yatakwenda kutoa elimu na kuihamasisha jamii kujitokeza katika uandikishaji.


## KUMBUKUMBU



**MZEE CONATUS VITALIS KAKOKO**
**Kuzaliwa: 19 Februari, 1938 - Kufariki: 08 Februari, 2019**

Ilikuwa ni tarehe 08 Februari, 2019 ulipotutoka, ikawa dakika, masaa, siku na hatimaye leo umetimiza mwaka mmoja (1) toka Baba yetu wa mbinguni akutwae kwenda kwenye makao yako ya milele. Ni vigumu kwetu kukubali kwamba haupo nasi kimwili, lakini tunafarijika kwa imani kwamba uko nasi kiroho na unaendelea kutuombea huko ulipo.
Matendo yako yatabaki daima ndani mwetu na amani na upendo uliotuachia vitaendelea kuwa mwongozo kwetu. Japo haupo nasi kimwili lakini kiroho bado tupo nawe. Baba, tulikupenda sana na tutaendelea kukupenda daima.

Unakumbukwa sana na mke wako mpendwa mama Margareth Kakoko watoto wako, Eng. Deusdedit, Eng. Col. Desiderius, Dkt. Deodatus na Mwalimu Devotha wakwe zako, wajukuu, vitukuu, ndugu, jamaa na marafiki

Familia ya Marehemu MZEE CONATUS VITALIS KAKOKO inawaalika kwenye misa ya kumbukumbu ya mwaka mmoja (1) tangu kifo chake itakayofanyika siku ya Jumamosi tarehe 08 Februari, 2020 saa 3 asubuhi nyumbani kwake marehemu kijijini Munjebwe, Rulenge-Ngara, Kagera.

**Mnakaribishwa sana,**
**BWANA ALITOA NA BWANA AMETWAA JINA LA BWANA LIHIMIDIWE, AMINA.**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Adhabu za waamuzi Bara zisisubiri 'kelele' za wadau

**WAKATI** mzunguko wa pili au hatua ya lala salama ya Ligi Kuu Bara inatarajia kuanza leo kwa mchezo mmoja kati ya vinara wa ligi hiyo na mabingwa watetezi, Simba dhidi ya 'Maafande' wa JKT Tanzania, kumekuwa na malalamiko mbalimbali kuhusiana na uwezo wa waamuzi.

Ligi Kuu ndio ligi ya juu ambayo hutoa mwakilishi au wawakilishi wa Tanzania Bara katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika, ambayo huchezwa kila mwaka chini ya usimamizi wa Shirikisho la Soka Afrika (CAF).

Ili kupata mwakilishi bora wa Tanzania Bara katika mashindano hayo, ni lazima timu au klabu zitakazopata tiketi ya kupeperusha bendera ya nchi zipatikane kwa haki na kwa uwezo.

Endapo bingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara atapatikana kwa 'mizengewe' au 'kubebwa' kama ilivyozoeleka, basi safari ya mwakilishi huyo huenda ikaishia njiani mapema pale itakapokutana na wapinzani wao ambao wameimarika na walipatikana kwa haki.

Katika siku za hivi karibuni, malalamiko kuhusiana na waamuzi wanaochezesha ligi hiyo yameongezeka, na malalamiko hayo yameonekana kujitokeza zaidi kwenye mechi zinazohusisha klabu kongwe nchini, Simba na Yanga.

Lakini ukiondoa timu hiyo, pia malalamiko kuhusu viwango vya waamuzi yamekuwa yakitolewa hata zinapokutana timu ndogo, lakini 'kelele' zake zinaonekana si kubwa kama zile zinazosikika kwa michezo inayohusisha Simba au Yanga, kwa sababu mechi hizo hazionyeshwi mubashara.

Inaelezwa katika mechi hizo zinazoitwa za timu ndogo, hali ni mbaya zaidi kwa sababu 'madudu' yanayodaiwa kufanywa ni ya kuidhalilisha ligi hiyo.

Kama hali hiyo ni kweli, umefika wakati wa viongozi wa Shirikisho la Soka Nchini (TFF) kwa kushirikiana na Bodi la Ligi Kuu Tanzania (TPLB) na Kamati ya Waamuzi kutosita kuchukua hatua kwa waamuzi na makamisaa ambao wataonyesha kiwango cha chini katika kazi yao.

Kuchukua hatua mapema, si mbali na kusaidia kupata bingwa aliyestahili, lakini pia kutasaidia kukuza kiwango cha soka nchini na baadaye Tanzania ikishuhudia timu zake zikifanya vizuri katika mashindano ya kimataifa na vile vile waamuzi hao kuteuliwa na CAF kuchezesha michuano mbalimbali inayofanyika barani Afrika.

Alhamisi tumeshuhudia Kamati ya Uendeshaji na Usimamizi wa Ligi ya Bodi ya Ligi Kuu Tanzania ikitoa adhabu kwa waamuzi waliochezesha mechi kati ya Simba dhidi ya Namungo na ile iliyohusisha Azam FC dhidi ya Prisons.

Kamati hiyo ilimfungia Mwamuzi msaidizi namba mbili, Kassim Safisha kwa muda wa miaka mitatu kwa kosa la kushindwa kutafsiri sheria ya kuotea kwa mujibu wa Kanuni namba 39(1)(a) ya Ligi Kuu kuhusu Udhibiti wa Waamuzi na ikimwandikia barua ya kukumbushwa majukumu, Mwamuzi Meshack Suda, lakini pia ikimuondoka kwenye orodha ya makamisaa, Abdallah Zongo kwa kosa la kutoa taarifa yenye upungufu.

Ili kuhakikisha Ligi Kuu Tanzania Bara inakuwa yenye heshima na hadhi, huu ni wakati wa TFF kuchukua hatua zinazostahili kwa kila atakayekwenda kinyume na kanuni na kwa kufanya hivyo, kutapunguza malalamiko ambayo yamekuwa yakiitia 'doa' ligi hiyo.

TFF isiendelee kuwapa adhabu waamuzi na maofisa wengine mbalimbali wanaovurunda bila kusubiri 'kelele' za wadau na kwa kufanya hivyo, itasaidia wahusika wote kuongeza umakini katika majukumu yao na mwisho wa siku, bingwa wa haki akapatikana na kikosi cha Timu ya Taifa (Taifa Stars), kinachotegemea wachezaji wengi kutoka kwenye ligi hiyo kupata nyota walioimara na walioandaliwa vema.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Waamuzi hawatendi haki

Na Barnabas Maro

**'MSIMAMIZI'** ni mtu mwenye dhamana ya kuangalia mwenendo wa shughuli maalumu; kulinda na kutunza mali. Mtu aliyepewa dhamana ya kusimamia watu wengine ili kuona kama wanafanya kazi itakiwavyo.

'Mwamuzi' ni mtu anayechezesha mpira uwanjani kulingana na sheria za mchezo; refa. Mtu anayeamua pande mbili zinazozozana ili kuzisuluhisha. Ni kama mahakama ambayo kesi husikilizwa na hakimu au jaji na kuitolea hukumu.

Kwa hiyo wasimamizi na waamuzi wanatakiwa kutekeleza (kitendo cha kukamilisha jambo lililopangwa; tenda kama inavyotakiwa) uamuzi wao bila kupendelea upande wowote hata kama upande mmoja unawahusu.

Wahenga walisema: "Kweli ingawa chungu niambie sinifiche." Maana yake niambie ukweli hata kama una uchungu. Methali hii tatufunza umuhimu wa kuwa na tabia ya kuusema ukweli au kuwa watu wausemao ukweli.

Kwa sababu hiyo, "Kweli ndio fimbo ya kukamata." Maana yake kweli ni silaha nzuri maishani. Twakumbushwa umuhimu wa kusema kweli hata kama kwa kufanya hivyo tutaishia kuchukiwa na watu. Ni wachache sana wanaokwenda viwanjani wakiwa na timu wanazozipenda. Narudia tena kusema ni wachache sana. Watazamaji wamegawanyika kwani kuna wanaokwenda kujiburudisha tu kwa kuwaangalia wachezaji wanaowapenda.

Katika hali hiyo, wapo mashabiki na wanachama wa timu tofauti wanaotoleana maneno ya kejeli na hata matusi! Penye wengi pana mengi.

Hata waamuzi na wasimamizi wana timu wanazozipenda, hasa tunapoziongelea Simba na Yanga. Ndo maana timu hizo wakati mwingine hupewa 'ushindi' usiokuwa wa haki zinapocheza na timu zingine!

Wanaofuatilia michezo ya timu za Simba na Yanga zinapocheza na timu zingine, na wenye kutaka haki itendeke ili kupata mshindi halali, watakubaliana nami kwa kutathimini michezo ya timu hizi mbili kwenye Ligi Kuu inayoendelea sasa. Sitaki kufukua makaburi. Naomba nieleweke hivyo. "Mtoto umleavyo ndivyo akuavyo." Kwa kawaida mtoto hukua jinsi alivyolelewa. Akilelewa vibaya ataishia kuwa na tabia mbaya. Methali hii hutumiwa kuwanasihi wazazi wawalee watoto wao vizuri ndipo wainukie kuwa na tabia nzuri na wawe watu wa kutegemewa.

Inadaiwa kuwa mechi za Simba na Yanga zina mambo matatu: 1) Kuwategemea waamuzi walio upande wao; 2) Rushwa wanazowapa waamuzi na hata baadhi ya wachezaji wa upande mwingine.

Hivi karibuni amekaririwa Kipa wa Yanga, Ramadhani Kabwili, akidai kiongozi fulani wa Simba aliahidi kumpa zawadi ya gari aina ya IST kama angefanya utovu wa nidhamu uwanjani utakaomsababishia aonyeshwe kadi ya tatu ya njano ambayo ingemfanya mchezo unaofuata dhidi ya Simba asicheze.Hapa kuna maswali yenye utata. Je, Kabwili aliwaeleza viongozi wa Yanga kuhusu rushwa aliyoahidiwa? Kama hakuwaeleza ni kwa nini na kama aliwaeleza, viongozi wake walichukua hatua gani? Kama nao waliamua kunyamaza, wana maana gani?

Je, aliiarifu Takukuru juu ya hilo? Kama hakuieleza ni kwa nini? Madai yake yataaminiwa vipi? Endapo atashitakiwa na Simba kwa kuchafua jina la klabu atakuwa na la kujitetea?

Twaambiwa "rushwa ni adui wa haki." Kama ndivyo, kwa nini (watoaji na wapokeaji) wanakumbatia rushwa?

"Ulimi huuma kuliko meno." Methali hii yatukumbusha kwamba maneno anayotamka mtu yanaweza kuumiza sana. Twashauriwa kupima maneno tusemayo kabla, ili yasije kuwaudhi na kuwakera wenzetu.

Jambo la tatu kuhusu Simba na Yanga linahusu ndumba (uganga wa kiasili wa kuponya au kudhuru; uchawi, ulozi, uramali; kipapai).

Kama viwanja vya serikali vina walinzi mahusus huwaje timu zikatae kwenda kwenye vyumba vya kubadilishia nguo? Upuuzi huu kamwe huwezi kuuona kwa wenzetu huko Uzunguni.

Imeandikwa: "Usiwe na miungu mingine ila Mimi." Amri ya kwanza ya Mungu inapiga marufuku kuheshimu miungu mingine zaidi ya Bwana mmoja aliyejifunua kwa Taifa lake. Inaharimisha ushirikina na utovu wa dini. Ushirikina kwa namna fulani huwakilisha upotofu wa dini unaopita kiasi: uovu wa dini ni kasoro ya kutokuwa na fadhila ya kidini.

"Ushirikina ni upotovu wa hisi za dini na wa matendo yanayotakiwa na hisi hizo. Waweza hata kuathiri uchaji tunaompa Mungu wa kweli. Mfano, mtu anapotoa umuhimu ulio wa kichawi, kwa namna fulani, kwa matendo fulani ambayo kwa yenyewe ni halali au ya lazima. Kuupa utendaji wa nje tu nguvu ya sala au ya ishara za sakramenti, nje ya hali za ndani zinayodaiwa, ni kutumbukia katika ushirikina.

"Ibada za miungu hazihusu tu ibada potofu za kipagani. Zinabaki kuwa kishawishi cha kudumu cha imani. Ibada za miungu ni kufanya mungu kile ambacho si Mungu.

"Binadamu huabudu miungu kila mara anapoheshimu kiumbe badala ya Mungu, iwe ni miungu au mapepo (mfano, ibada ya mashetani), nguvu, furaha, taifa, mababu, serikali, fedha n.k."

**marobarnabas@yahoo.com**
**0784 334 096**

HABARI KITAIFA

# Ataka mabadiliko ya kiutendaji wizarani

**Na Mwandishi Wetu,**
DODOMA

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mary Makondo, amewataka watumishi wa sekta ya ardhi katika wizara hiyo kushirikiana ili kuibadilisha wizara na kuwa na utendaji bora utakaokidhi mahitaji ya wananchi.

Makondo alisema hayo jana wakati akizungumza na watumishi wa wizara hiyo alipowasili kwa mara ya kwanza baada ya kuteuliwa na Rais John Magufuli kushika wadhifa huo.

Amechukua nafasi hiyo iliyoachwa na Dorothy Mwanyika aliyestaafu kwa mujibu wa sheria. Kabla ya uteuzi huo, Makondo alikuwa Kamishna wa Ardhi katika Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Alisema mategemeo ya watumishi wa wizara mara baada ya kuteuliwa kwake ni makubwa, lakini msisitizo wake ni watumishi hao kufanya kazi kwa bidii na kwa kujituma ili kuibadilisha wizara.

“Kauli ya wizara kuwa ina ‘madudu’, siyo nzuri, hivyo tukimbie ili tuwe na sekta ya ardhi iliyobadilika” aliagiza.

Aliwataka kuthamini mchango wa kila mtumishi wa wizara hiyo kwa kuwa ndiyo njia pekee itakayoleta mabadiliko na mafanikio ya utendaji kazi wa sekta hiyo.

Kwa mujibu wa Makondo, kampuni ya utengenezaji magari ya Toyota imefanikiwa kwa kiasi kikubwa kwenye biashara zake kutokana na kutumia mfumo wa Kaizen unaothamini mchango wa kila mmoja katika utendaji kazi.

Makondo aliwataka watumishi wa wizara kuweka mikakati ya pamoja kwa lengo la kuibadilisha wizara hapo ilipo na kuonyesha imebadilika katika utendaji wake.

Baadhi ya watumishi wa wizara hiyo walieleza kufurahishwa na uteuzi wa Katibu Mkuu huyo kwa kuwa ametokea wizara hiyo na anaijua sekta ya ardhi vizuri pamoja na watumishi wake.




Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mussa Azzan Zungu (kushoto), akishuhudia wakati Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dk. Samuel Gwamaka (wa pili kushoto), akikabidhi cheti cha tathmini ya athari kwa mazingira kwa Mtendaji Mkuu wa TOTAL, Martin Tifany, kwa ajili ya mradi wa bomba la kusafirisha mafuta ghafi la Afrika Mashariki (EACOP), jijini Dodoma juzi. **PICHA: OMR**

# Biteko: Hakuna konakona utoaji wa leseni za madini

**Na Mwandishi Wetu,**
DODOMA

WAZIRI wa Madini, Doto Biteko, amesema utaratibu wa upatikanaji wa leseni za madini za aina mbalimbali hupatikana kwa mujibu wa sheria na taratibu na kusisitiza kwamba hakuna ubaguzi katika utekelezaji wa suala hilo.

Amesema utoaji huo wa leseni huzingatia masharti na atakayeshindwa, sheria hutumika ikiwamo kutoa hati ya makosa na hatimaye kuifuta.

Biteko aliyasema hayo juzi wakati wa kikao chake na kampuni ya Peak Resources Ngwala (PRNG) ofisini kwake jijini hapa, akizungumzia masuala ya utoaji wa leseni za uchimbaji madini.

Kampuni hiyo ilikuwa ikifuatilia upatikanaji wa leseni ya uchimbaji madini na Biteko alisema suala lao linashughulikiwa na taratibu zikikamilika watapatiwa.

Alisema kwa wakati wa sasa suala la leseni si kificho na halihitaji kumwona mtu ili apate leseni bali kikubwa ni kufuata utaratibu uliowekwa na kuzingatia sheria. Alisisitiza kuwa kampuni hiyo itapata leseni pindi taratibu zitakapokamilika.

Mkurugenzi Mtendaji wa PRNG, Luca Stanfield, alimshukuru waziri kwa mazungumzo yake huku akisema wanasubiri kupata leseni ili waanze kazi na watafuata sheria.

Biteko amesema leseni zinatolewa kwa kila mtu iwe wa ndani au nje ya nchi lakini kila mhusika anapaswa kuzingatia sheria na taratibu.

“Kwenye utoaji wa leseni kuna sheria za kuzingatia ikiwamo ulipaji tozo za kodi za serikali ambazo mwombaji anapaswa kuzifahamu na kulipa,” alisema Biteko.

# Zungu asema mradi bomba mafuta salama

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mussa Zungu, ameshuhudia makabidhiano ya cheti cha tathmini ya athari kwa mazingira kwa mradi wa bomba la kusafirisha mafuta ghafi la Afrika Mashariki ikiwa ni hitimisho la ripoti ya tathmini ya mazingira kwa mradi huo.

Katika makabidhiano hayo jana, Zungu alisema mradi huo wa bomba lenye urefu wa km 1,443 kutoka Wilaya ya Hoima, Uganda hadi eneo la Chongoleani katika Bandari ya Tanga hauna athari hasi kwa mazingira.

Alibainisha kwa upande wa Tanzania pekee, bomba lina urefu wakilomita km 1,114 ambao ni asilimia zaidi ya asilimia 80 ya mradi, zitakazopita katika mikoa mnane na wilaya 24 nchini.

“Furaha yangu inatokana na uhalisia kwamba sehemu kubwa ya mradi na vituo viko Tanzania na NEMC wameweza kufanya kazi hii na kumaliza kwa wakati.

“Upande wa Uganda bado wako kwenye hatua za mwisho. Natumaini hafla hii itawahimiza watendaji na mamlaka za wenzetu kuweza kukamilisha tathmini hizi za mazingira kwa wakati,” alisema.

Alisema hafla ya kukabidhi cheti cha tahtmini hiyo, ni ushahidi wa serikali imeridhia mradi huu kuhakikisha masuala ya kiuchumi, kijamii, mazingira, afya na usalama yanashughulikiwa wakati wote wa kipindi cha kupanga, kujenga na uendeshaji wa shughuli za bomba.

“Ili kupunguza athari kwa mazingira na jamii, njia litakapopita bomba, vituo vitawekwa na kuendeshwa kwa umakini ili kupunguza athari yoyote ya kimazingira na kiikolojia,” aliahidi.

Waziri Zungu alisema kazi ya serikali kupitia NEMC haiishii kutoa cheti tu, bali kuendelea kufuatilia na kutathmini utekelezaji wake kulingana na masharti ya cheti kilichotolewa.

Waziri wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, alisema hatua tano za awali zimekamilika katika utekelezaji wa mradi huo ikiwa ni pamoja na upakatikanaji wa eneo la kujenga matenki manne yenye uwezo wa kuhifadhi lita laki 2.5, kulipa fidia kwa wakazi wa eneo litakalohusika na mradi huo, utafiti wa kijiolojia na fizikia na tathmini ya fidia kwa watakaopisha eneo katika korido ambayo itapita katika mikoa minane na wilaya 24.

Utekelezaji wa mradi huo unafanywa na kampuni ya Total East Africa.

# Wenye madeni TRA wapata msamaha

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

HATIMAYE Bunge limekubali kufutwa rasmi kwa madeni ya nyuma ya ada na leseni za magari, riba na adhabu kwa zaidi ya wadaiwa 365,000 nchini.

Jana, Bunge liliridhia kufutwa rasmi kwa madeni ya wadaiwa hao ambayo yanafikia zaidi ya Sh. Bil. 398.4.

Bunge lilielezwa kuwa uamuzi huo unalenga kupunguza mlundikano wa hoja za ukaguzi ambazo zilikuwa zinajirudia mwaka hadi mwaka kutokana na kutofanyika kwa marekebisho katika vitabu vya serikali.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC), Naghenjwa Kaboyoka, aliyasema hayo wakati akiwasilisha maoni ya kamati yake kuhusu azimio hilo.

"Bunge limepewa mamlaka ya kufuta madai au hasara zinazotokana na upotevu wa fedha na vifaa vya serikali, hivyo ni jukumu la kamati kwa maelekezo ya kamati ya uongozi ya Bunge kujiridhisha na sababu na umuhimu wa kufuta hasara au upotevu husika, kabla ya kupendekeza kwa Bunge kuzifuta. "Baada ya uchambuzi huo, kamati inaunga mkono azimio la kufuta na kusamehe hasara ya maduhuli ya Sh.398,445,888,750 inayotokana na kufutwa kwa madeni ya nyuma ya ada ya leseni za magari na msamaha wa kodi, riba na adhabu husika," alisema

Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, aliwasilisha kwenye kamati hiyo hasara ya maduhuli ya fedha za serikali kwa kipindi kilichoishia Juni 30, 2019.

Alisema serikali ilichukua uamuzi wa kufuta ada hiyo baada ya kutafakari juu ya magari mengi ambayo yalikuwa mabovu na hayatembei. Aidha, serikali ilitoa msamaha wa kodi, riba na adhabu zinazoambatana na madeni yote ya ada hiyo yaliyolimbikizwa miaka ya nyuma.




Gari lenye namba za usaji T 511 CET, likiwa limeanguka katika mtaro, baada ya dereva wake kushindwa kulimudu katika eneo la Kivule, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Ajali ya basi, lori yajeruhi 10

INATOKA UK. 4

lilikuwa kwenye mwendo mkali na kugongana uso kwa uso.

"Kulikuwa na lori limeharibika na kuegeshwa barabarani, na mbele yake lilikuwapo lori lingine aina ya fuso, sasa hili lori lilianza kulipita lori bovu na wakati linaanza kulipita fuso, ndipo nikaona basi limekuja kwa mwendo mkali yakagongana," alidai.

Alidai dereva wa basi alikuwa na mwendo mkali ambao asingeweza kusimama kusubiri malori yapishane na ndiyo sababu magari hayo yakagongana.

Mmoja wa majeruhi wa ajali hiyo, Emmanuel Paulo, alidai basi hilo lilikuwa kwenye mwendo mkali likifukuzana na gari lingine walilokuwa wamelipita na walishtukia tu gari lao likipepesuka na kusimama na alipoteza fahamu na alipozinduka akajikuta yuko hospitalini akitibiwa.

"Ninachokumbuka ni kwamba basi letu lilikuwa likifukuzana na basi lingine, tukalipita na tukiwa kwenye mwendo huo mkali, nilistukia gari letu linayumba na kusimama, niliona upande wa dereva pakiwa wazi na watu wanapiga kelele, nikapoteza fahamu na nilipozinduka nimejikuta nikiwa hapa hospitalini," alisimulia.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, ambaye pia ni Diwani wa Inyara, alikuwa kiongozi wa kwanza kufika kwenye eneo hilo la ajali na kusema kuwa amesikitishwa na ajali hiyo ambayo ilionyesha kuwa watu wengi wameumia na pengine vifo vingetokea.

Alidai ushahidi wa awali kutoka kwa mashuhuda unaonyesha kuwa chanzo cha ajali hiyo ni mwendokasi wa basi la Kampuni ya Premier, hivyo akawasihi madereva kuendesha kwa mwendo unaokubalika kisheria ili kuepusha ajali kama hizo.

"Nimesikitika kwamba ajali hii imetokea katika eneo langu la uongozi, lakini kwa vile ushahidi kutoka kwa mashuhuda unaonyesha chanzo chake ni mwendokasi, mimi nitoe wito kwa madereva kuendesha magari kwa mwendo wa kawaida ambao unakubalika kisheria ili kuepusha ajali kama hizi," alishauri.

Alisema baada ya kupata taarifa ya ajali hiyo alitoa taarifa kwa Jeshi la Polisi na askari wakafika haraka kuhakikisha eneo hilo, majeruhi na mali za wananchi zinakuwa salama, ikiwa ni pamoja na kutoa huduma za haraka kwa watu waliopatwa na ajali.

"Kikubwa nashukuru Mungu kwamba askari wamewahi na kuanza kuokoa roho za watu ambao walikuwa wamepata ajali kwa kuwanasua kutoka kwenye gari na kuwakimbiza hospitali ambako sasa hivi wanaendelea kupata huduma za matibabu," alisifu.

Daktari wa zamu katika Kitengo cha Dharura cha Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Mbeya, Dk. Olivia Masoi, alithibitisha kupokea majeruhi 10 na kusema kuwa hakuna mtu aliyekuwa amepoteza maisha kwenye ajali hiyo.

Alisema awali kuna watu wawili walidhaniwa kuwa walipoteza maisha wakiwa kwenye eneo la ajali, lakini walipofikishwa hospitalini hapo na kuchunguzwa, walibaini kuwa watu hao wangali hai na ndipo wakawahishwa katika chumba cha wagonjwa mahututi.

Alisema watu hao kwa sasa wako chini ya uangalizi wa karibu kutoka kwa madaktari bingwa na kwamba hali zao zinaendelea vizuri. Alisema kuwa miongoni mwa majeruhi waliowapokea hospitalini hapo, kati yao sita na miongoni mwa wanawake hao, mmoja ni mtoto.

## CCM yaonya wanaonunua uongozi

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MWENYEKITI wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Mkoa wa Arusha, Zelothe Steven, amewataka wananchi wa mkoa huo kuwa makini na fedha wanazopatiwana watu wanaonyemelea uongozi katika kipindi hiki kuelekea uchaguzi mkuu.

Akitoa tahadhari hiyo jana katika ziara ya ukaguzi wa miradi inayotekelezwa na Halmashauri ya Jiji la Arusha, ikiwa sehemu ya maadhimisho ya miaka 43 ya kuzaliwa kwa chama hicho, Zelothe alisema kumekuwa na tabia ya baadhi ya watu kununua binadamu wenzao kama chumvi kwa kuwadanganya kwa Sh. 5,000 au 10,000 ili wachaguliwe.

"Naomba akitokea mtu huyo kwenu mwogopeni kwa sababu akikununua, akishakupata kwamba amekununua, baada ya wewe kusema ndiyo, kitakachofuata kwako ni hapana. Nenda gonga mlango wake, piga simu yake, hupati majibu kwa sababu hana muda anataka kurejesha alichopoteza,"alisema.

Alisema atakayepita pita kwa misingi hiyo, wachukue hata kamba za migomba wamfunge na kumpelekea ili awachukulie hatua stahiki.

Pia alisema katika kinyang'anyiro cha uchaguzi mwaka huu, hatampitisha mtu kwa misingi ya kubeba watu kwa kuwa hana mtoto wa mgongoni, kichwani, mfukoni wala tumboni.

"Mimi nitatenda haki kwa sababu nikikosea tu mjue kule mbele ataenda kukutana na kina Mzee Philip Mangula, kule hakuna utani na mimi sitaki kuulizwa ilikuwaje nimepeleka mtu wa namna hii. Kila mtu afuate taratibu na nitakua makini kweli kweli katika hili,"alisema.

Sambamba na hilo, aliwaomba wananchi hao katika uchaguzi wa mwaka huu, kuhakikisha wanapochagua viongozi, hawaingizi mbu hata mmoja ndani ya nyumba.

"Hongereni, mmejenga msingi mzuri kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa. Sasa kilichobaki mjenge ukuta na madirisha msilibe vizuri, ili mbu asiingie hata mmoja na ikitokea ameingia mbu mmoja, tafuteni ugoro mummwagie huyo mbu," alisema.



Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi (CCM), Mkoa wa Arusha, Zelothe Stephen (kushoto), akikagua ujenzi wa maabara Shule ya Sekondari Oldonyowas juzi, wakati wa ziara ya kamati ya siasa mkoani humo, ya kukagua miradi ya maendeleo ikiwa ni utekelezaji wa Ilani ya CCM kwa miaka minne ya serikali ya awamu ya tano. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# Jaji ataka nakala za hukumu ndani ya siku 21

**Na Allan Isack,** ARUSHA

JAJI Mfawidhi wa Mahakama Kuu Kanda ya Arusha, Moses Mzuna, amewataka majaji na mahakimu wa mahakama mkoani hapa, kutoa nakala za hukumu za kesi kwa wananchi ndani ya siku 21.

Akizungumza wakati wa maadhimisho ya Siku ya Sheria, Jaji Mzuna alisema kumekuwa na malalamiko kutoka kwa wananchi kuwa wanachelewa kupewa nakala za hukumu mahakamani.

"Naomba majaji na mahakimu wa mahakama mtoe nakala za hukumu kwa watu ndani ya siku 21," alisema Mzuna. Licha ya kuzungumza hayo, alisema Mahakama imejiwekea malengo ya kutoa haki kwa wakati.

Alisema kila Jaji anatakiwa kumaliza mashauri 220 kwa mwaka, kila hakimu mkazi wa mkoa na wilaya anatakiwa kumaliza mashauri 250 kwa mwaka na mahakimu wa mahakama za mwanzo mashauri 260 kwa mwaka.

Pamoja na kujiwekea utaratibu huo, alisema watahakikisha mashauri hayachukui muda mrefu wala kuahirishwa pasipo kuwa na sababu za msingi.

"Maelekezo ya sasa katika mahakama za mwanzo hayapaswi kukaa zaidi ya miezi sita, mahakama ya hakimu mkazi miezi 12 na Mahakama Kuu miaka miwili," alisema.

Kwa mujibu wa Jaji Mzuna, Mahakama Kuu Kanda ya Arusha mwaka 2018 yalimalizika ndani ya siku 347 na mwaka 2019 yalimalizika ndani ya siku 397, hivyo imefanya kwa vipindi vyote mashauri kumalizika kwa mwaka na mwezi mmoja.

Hata hivyo, alisema Mahakama ya Tanzania imeanzisha divisheni maalumu ya inayoshughulikia mashauri ya biashara na uwekezaji kwa lengo la kuhakikisha mashauri yanaamuliwa kwa ufasaha ili kuchochea biashara na uwekezaji nchini.

"Masijala ndogo ya Arusha imeanzishwa mwaka 2004 tangu kuanzishwa kwake imepokea mashauri 328 na kati ya hayo, yaliyosikilizwa ni 304 na yaliyobaki ni 24.

Alisema katika dhana ya utoaji haki kwa wakati na kukuza uchumi na biashara Mahakama ya Tanzania imeingia makubaliano na wadau mbalimbali kufikia malengo ya Mahakama. Pia alisema katika kutambua umuhimu wa mahakama katika jukumu la kuweka mazingira wezeshi kwa biashara na uwekezaji, bunge lilipitisha mabadiliko ya sheria namba 3 ya mwaka 2018 ili kuiwezesha mahakama kuamua mashauri kwa kuzingatia kiini cha mgogoro na si taratibu za kiufundi.

Mwendesha Mashtaka Mkuu Ofisi ya Taifa ya Mashtaka Mkoa wa Arusha, Abdala Chavula, alisema kuwapo kwa mfumo huru wa haki jinai katika ukuaji wa uchumi unaongeza usalama kwa wananchi na kupunguza uhalifu na gharama za kiuchumi kwa serikali.

Alisema mfumo huo unaleta amani na utulivu katika jamii, hivyo shughuli za uwekezaji na biashara zinafanyika kwa wepesi.

Pia alisema mfumo dhaifu wa haki jinai huongeza wimbi la uhalifu ikiwemo vitendo vya rushwa,ukwepaji kodi,matukio ya kigaidi, ujambazi, wizi, uporaji, vitendo vya ulaghai na wizi kwa njia ya mtandao na utapeli.

# Mwenyekiti ataka serikali iungwe mkono

**Na Allan Isack,** ARUMERU

MWENYEKITI wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Arusha, Zelothe Steven, amewatakata wananchi katika Halmashauri ya Arusha DC, wilayani Arumeru, kuunga mkono juhudi za serikali za katika kutekeleza miradi ya maendeleo.

Zalothe aliyasema hayo juzi wakati wa ziara ya Kamati ya Siasa Mkoa wa Arusha kwa ajili ya kukagua miradi ya maendeleo wilayani hapa.

Alisema wananchi wanatakiwa kuunga mkono utekelezaji wa miradi ya sekta za elimu, afya, maji, kama ilivyokuwa azma ya serikali kufikia uchumi wa kati na viwanda ifikapo mwaka 2025.

Mwenyekiti huyo alisema ziara hiyo imelenga kukagua utekelezaji wa Ilani ya CCM kwa kipindi cha miaka minne tangu walipoingia madarakani.

Zelothe alisema serikali imeleta mabadiliko makubwa ya kimaendeleo kwa wananchi, ikiwamo kutekeleza miradi mingi kwa muda mfupi, kulinganisha na awamu zilizopita.

Hata hivyo, amewapongeza wananchi wa vijiji vya Oldonywas, Mbuyuni na Nduruma kwa kujitoa kuchangia nguvu zao na kufanikisha utekelezaji miradi hiyo.

Licha ya wananchi kuchangia nguvu kazi na serikali imetoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa miradi hiyo.

"Nimeridhishwa na taarifa za miradi yote niliyotembelea na kamati yangu tumeona wananchi walivyochangia kwa asilimia 10 katika utekelezaji wa miradi hii," alisema Zelothe.

Miradi aliyotembelea ni upanuzi wa kituo cha afya Mbuyuni katika Kata ya Oljoro, na mradi huo umegharimu Sh. milioni 400, upanuzi wa kituo cha afya Nduruma Sh. milioni 500 na ujenzi wa Shule mpya ya Sekondri Oldonyowas, uliogharimu Sh. milioni 709.3.

# Kompyuta zatolewa kupunguza ukatili

**Na Allan Isack,** ARUSHA

SHULE nane za sekondari katika wilaya za Monduli na Ngorongoro mkoani Arusha, zimepewa kompyuta ndogo 80 (tablet), zilizowekewa mfumo maalumu wa kutoa na kupokea taarifa zinazohusu ukatili wa kijinsia kwa wanawake na wasichana.

Mfumo huo hautakuwa na gharama yoyote kwa watumiaji kwa kuwa utakuwa ukitumiwa bila kuwa na kifurushi cha data.

Katibu Tawala Mkoa wa Arusha, Richard Kwitega, akizungumza wakati wa ugawaji wa kompyuta hizo katika mji mdogo wa Mto wa Mbu, alisema mradi huo unatekelezwa na shirika lisilo la kiserikali la Pastoral Women's Council (PWC), maarufu kwa jina la Tapala.

Alisema lengo la mradi huo ni kuzuia matukio ya unyanyasaji kwa wanawake na wasichana yanayoendelea katika jamii.

Kwitega alisema mradi huo unatekelezwa katika vijiji vinane vya jamii ya wafugaji kwa kipindi cha miaka mitano na unafadhiliwa na shirika la kimataifa la Ubelgiji la Trias.

Alisema shirika hilo lilianzisha mradi huo kwa ajili ya kuwasaidia wanafunzi 3,000, walimu 120, viongozi wa mitaa na jamii wanaozunguka shule hizo.

"Ukatili wa kijinsia ni vitendo viovu vinavyozalilisha watu vinavyotesa, vinavyonyanyasa, vinavyokandamiza na havijali haki za kuishi kwa binadamu na ukatili unaweza kufanywa kwa watoto wa kiume au kike," alisema Kwitega.

Licha ya kuzungumza hayo alisema utafiti unaonyesha kuwa ukatili wa kijinsia ni tatizo kubwa linaloikabili dunia kwa sasa hususani katika nchi mbalimbali zinazoendelea.

"Kwa mujibu wa utafti wa Shirika la Afya Duniani (WHO) za mwaka 2013, takribani asilimia 35 ya wanawake duniani wamefanyiwa ukatili wa kijinsia wa kupigwa au kubakwa katika maisha yao," alisema Kwitega.

"Nchi yetu ni miongoni mwa nchi ambazo zinakabiliwa na tatizo la ukatili wa kijinsia na takwimu zilizotolewa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu ya mwaka 2015/16 kupitia taarifa ya idadi ya watu na afya, inakadiriwa kuwa asilimia 40 ya wanawake wenye umri kati ya miaka 15 hadi 49, wamefanyiwa ukatili wa kijinsia wa aina mbalimbali," aliongeza.

Mkurugenzi wa Trias Kanda ya Afrika Mashariki, Bart Casier, alisema lengo la mradi huo ni kuungana na juhudi za serikali katika kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na wasichana.

"Mkutano huu ni muhimu sana kwani vita dhidi ya ukatili wa mwanamke na mtoto wa kike si rahisi, kunahitajika kutokomeza matukio haya ili kujenga mpya na yenye kuheshimiana," alisema Casier.

Ofisa Ustawi wa Jamii Mkoa wa Arusha, Denis Mgiye, alisema matukio ya ukatili wa kijinsia mkoani humo kwa takwimu za Julai hadi Septemba, mwaka jana, jiji la Arusha linaongoza kwa matukio 427, Arusha DC matukio 371, Meru matukio 93, Monduli matukio 136, Karatu 186, Longido 101 na Ngorongoro 34.



Baadhi ya wanafunzi walemavu na watu wazima wenye tatizo hilo kutoka Kata ya Makojo, wakiwa na baadhi ya vitu walivyopewa msaada na Mradi wa kusaidia watu wenye ulemavu na wanafunzi wa BMZ wa serikali ya Ujerumani, katika ofisi zake katika Hospitali Teule ya Shirati wilayani Rorya mkoani Mara juzi. BMZ imetoa vifaa vya shule na vyakula vyenye thamani ya Sh. milioni 16 kwa kata 10 za wilaya ya Musoma. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Utunzaji skimu za umwagiliaji tatizo

**Na Mary Mosha,** MOSHI

LICHA ya serikali kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji kuendeleza miundombinu ya umwagiliaji katika skimu mbalimbali, miundombinu hiyo bado haitunzwi kama inavyotakiwa.

Miundombinu hiyo imekuwa ikiendelezwa kwa kushirikiana na Shirikia la Maendeleo la Japan (Jica) katika maeneo mbalimbali nchini.

Hayo yalisemwa juzi mjini hapa na Mhandisi wa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji Mkoa wa Kilimanjaro, Said Ramadhani alipokuwa akizungunza na wanahabari ofisini kwake.

Alisema uendeshaji na utunzaji wa miundombinu ya umwagiliaji umekuwa hauridhishi kutokana na uelewa mdogo wa wakulima juu ya matunzo, hali hiyo imekuwa ikisababisha skimu nyingi kukosa tija kwa kutodumu muda mrefu licha ya kutumia gharama kubwa wakati wa ujenzi wake.

"Wadau wote wanaohusika wanatakiwa kutoa elimu kwa wakulima mara kwa mara ili kuhakikisha skimu hizo zinakuwa endelevu ili kuleta tija, kuwa na uhakika wa chakula na kupunguza umaskini kuanzia ngazi ya familia hata taifa kwa ujumla," alisema. Ramadhani alisema ni wajibu wa kila umoja wa wamwagiliaji kuhakikisha unasimamia ukusanywaji wa asilimia tano ya mapato kwa kila mwanachama katika skimu kwa ajili ya shughuli za uendeshaji na matunzo ili skimu ziwe endelevu kama ilivyoainishwa katika Sheria ya Umwagiliaji Namba 5 ya Mwaka 2013.

"Wataalamu wa kilimo kuanzia ngazi ya skimu, kijiji hadi mkoa wana wajibu wa kuhakikisha utekelezaji wa sheria hii unazingatiwa ili kuleta tija kwenye skimu hizo ikiwa ni pamoja na matengenezo madogo madogo.

"Katika kutekeleza majukumu ya uendelezaji na utunzaji wa skimu za umwagiliaji ili ziwe endelevu, wataalamu kwa kushirikiana na wakulima wanatakiwa kufuata mwongozo kabambe wa umwagiliaji," alisema.

Mmoja wa wanakijiji katika Skimu ya Mtambo, Jumanne Idd, alisema bado hakuna elimu ya kutosha juu ya utunzaji wa miundombinu inayotengwa na Tume ya Taifa ya Umwagiliaji.

Naye Ofsa Umwagiliaji wa Wilaya ya Hai, John Chuwa, alisema mbali na kuwapo kwa changamoto hizo bado wanaendelea kutoa elimu kwa wakulima ili kuleta mabadiliko katika sekta ya kilimo.

## Watakiwa kuunda kamati za usalama

**Na Mary Mosha,** MOSHI

WANANCHI wa Kata ya Shirimatunda Manispaa ya Moshi, wametakiwa kuwa chachu ya usalama katika eneo lao kwa kuanzisha kamati za ulinzi na usalama ili kukomesha vitendo vya wizi vilivyoshamiri.

Diwani wa Kata hiyo, Francis Shio, alisema hayo jana katika mkutano wa maendeleo na wananchi uliofanyika katika ofisi za kata hiyo mjini hapa.

Shio alisema suala la wizi katika Kata ya Shirimatunda limezidi kushamiri kutokana na hali ya uchumi kubadilika na watu wanarahisisha maisha kwa kujipatia kipato kwa njia ya wizi jambo ambalo limesababisha kutoweka kwa hali ya usalama.

"Hali ya uchumi kwa sasa imebadilika na mfumo wa maisha ni lazima ubadilike. Watu wanajitafutia kipato kwa njia za wizi, ni lazima wananchi mjitoe kuanzisha kamati za usalama ili kukomesha wimbi la wizi linaloimaliza kata yetu," alisema Shio.

Aidha, Shio aliwataka wananchi kutojenga katika hifadhi za barabara ili kuepuka usumbufu na hasara ya kubomoa majengo hayo wakati wa kupisha ujenzi wa miundombinu ya barabara.

Inspekta wa Polisi Kanda ya Moshi Magharibi, David Gabriel, aliwataka wananchi kuacha itikadi za vyama na dini na kuwataka kuwa pamoja katika kuhakikisha usalama unapatikana katika Kata hiyo.

Alisema suala la ulinzi ni nyeti kwa kuwa kusipokuwa na usalama katika jamii husika, wananchi watashindwa kujihusisha na shughuli za kimaendeleo.

Mmoja wa wananchi katika kata hiyo, Joseph Mushi, alisema suala la wizi limekithiri katika kata hiyo na kusema ikiwa watapewa mwongozo sahihi wa namna ya kuanzisha kamati hizo za ulinzi na usalama, wanaweza kutokomeza matukio ya kihalifu.

# Wataka elimu kuhusu saratani iwe ajenda kuu katika mikutano

**Na Mary Mosha,** MOSHI

WANANCHI wa Mkoa wa Kilimanjaro wameiomba serikali kuangalia uwezekano wa kuendelea kutoa elimu juu ya saratani ya tenzi dume ili kuhakikisha wanaume wanajitokeza kwa wingi katika kupima afya zao.

Mmoja wa wananchi hao, Sabastian Msofe, alisema juzi kuwa bado wananchi hawana elimu ya kutosha juu saratani ya tenzi dume hali inayowafanya kuchelewa kufika kwenye matibabu jambo ambalo husababisha kupoteza maisha.

Alisema bado katika jamii kuna imani potofu juu ya tenzi dume hali ambayo serikali inapaswa kuingilia kati hasa katika kutoa elimu katika kila mikutano ya vijiji na kata. Pia alishauri viongozi wa dini nafasi zao kutoa elimu juu ya suala hilo.

Naye Raphael Elisante alisema: "Tunaiomba serikali kutoa agizo kwa wataalamu kwanzia ngazi za vijiji kufika kwa kila mkutano wa kijiji, kata, wilaya na hata mkoa kutoa elimu ya afya ya kuzungunzia magonjwa ya saratani hasa tenzi dume ili kuleta afueni kwa wanaume."

Alisema ikiwa viongozi katika ngazi mbalimbali watapewa agizo kuhakikisha wanaweka agenda ya afya katika mikutano yao, jambo hilo litawezekana na wengi watajitokeza. "Halmashauri pia itume mtaalamu wa afya kufika na kuelezea magonjwa ya saratani. Hii itasaidia kubadilisha maisha ya Watanzania na kupata taifa la watu wenye afya bora ambao wataweza kuleta maendeleo," alisema.

Grace Lucas, mkazi wa Wilaya ya Siha, alisema katika baadhi ya makabila wamekuwa wakiogopa kwenda kupima na hata wakigundulika kuwa na saratani hiyo wamekuwa wakikaidi kutumia dawa hali ambayo imekuwa chanzo cha vifo vya mara kwa mara kwa wanaume

Naye daktari bingwa wa magonjwa ya saratani ya tenzi dume katika Hospitali ya Rufani ya Kanda ya KCMC, Necolus Ngowi, alisema bado mwamko ni mdogo kwa jamii katika upimaji wa afya.

"Ikiwa serikali italichukulia hilo kama agenda kuu katika mikutano yake, tutaweza kuisaidia jamii ya Watanzania," alisema.

Dk. Ngowi alisema watu wanaopata ugonjwa huo mara nyingi ni kinababa wenye umri kwanzia miaka 40.

"Ni kweli mwamko bado ni mdogo kwa sababu wananchi hawana elimu ya kutosha lakini kwa kushirikiana na serikali na mashirika binafsi, tutawasaidia wanaume wengi na kuokoa maisha yao kwani saratani yoyote ikiwahiwa inatibika," alisema Dk. Ngowi.



# Jaji ahimiza haki kortini

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

JAJI Mfawidhi wa Mahakama Kuu Kanda ya Dodoma, Mustafa Siyami, amezitaka mahakama nchini kutoa haki kwa wakati ili wananchi wenye mashauri yao ya kibiashara yaamuriwe mapema badala ya kutumia muda mwingi kusikiliza kesi zao.

Jaji Siyami aliyasema hayo juzi katika maadhimisho ya Siku ya Sheria nchini yaliyofanyika kwenye Uwanja wa Mahakama Kuu jijini hapa.

Alisema kumekuwa na ucheleweshaji usiokuwa wa lazima wa mashauri mahakamani na kuwataka mahakimu kuzingatia kanuni na miongozo ya muda uliowekwa wa kuanzia kusajili kesi hadi kutolewa hukumu uliowekwa na Mahakama Kuu. "Muda ni kitu cha thamani sana kwa mfanyabiashara na mwekezaji, kwa hiyo ni lazima mashauri yanayohusu kesi za biashara na uwekezaji yasichukue muda mrefu kutolewa hukumu ili nchi yetu ifikie uchumi wa kati," alisema.

Aliongeza kuwa kauli mbiu ya maadhimisho ya siku ya sheria mwaka huu inataka mahakama kuwa kiungo kikubwa cha kutoa haki kwenye mashauri yanayohusu biashara na uwekezaji kwa kutoa hukumu kwa wakati bila kuchelewesha ili wafanyabiashara hao waendelee na majukumu.

Alibainisha tofauti na mashauri mengine yanayofikishwa mahakamani, Mahakama Kuu imeanzisha kitengo maalum cha kusikiliza mashauri yanayohusu biashara na uwekezaji yasiyozidi miezi 10 tangu kusajiliwa hadi kutolewa hukumu. Mwendesha Mashtaka wa Serikali Mkoa wa Dodoma, Pius Hilla, alisema Mkoa wa Dodoma una kiwango kidogo cha uhalifu kulinganisha na mikoa mingine.

Alisema pamoja na mkoa huo kuwa na kiwango kidogo cha uhalifu, ujio wa serikali mkoani hapa umeanza kuongeza matukio ya uhalifu katika kila sekta ikiwamo udanganyifu katika masuala ya ardhi, utapeli katika miamala ya fedha, utapeli kwa kutumia mitandao, uvunjifu wa haki za binadamu, hasa mauaji na ujangili.

Aliitaka mahakama kupambana na uhalifu huo kwa kutoa adhabu kali kwa watu watakaopatikana na hatia kwa mujibu wa sheria.

Mwenyekiti wa Chama cha Wanasheria wa Tanganyika (TLS) Mkoa wa

Dodoma, Mary Munisi, alisema ni utawala bora pekee nchini ndiyo utakaowavutia wawekezaji kuja kuwekeza na si vinginevyo.

Alisema mahakama kwa kushirikiana na mihimili mingine nchini imejipanga kuweka mazingira mazuri kwa ajili ya wafanyabiashara na wawekezaji kutoka nje kwa kuwa bila utawala bora hakuna mwekezaji atakayekuja kuweka fedha zake mahali ambapo hakuna usalama.

# Ukaguzi mikataba madereva waja

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imesema itafanya ukaguzi kubaini madereva wa magari makubwa na madogo nchini ambao hawapewi mikataba na wamiliki wa vyombo vya moto.

Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana na Ajira, Anthony Mavunde, aliyasema hayo bungeni jijini Dodoma jana alipokuwa akijibu swali la nyongeza la Mbunge wa Nyamagana (CCM), Stanslaus Mabula.

Mbunge huyo alisema pamoja na kazi nzuri ua urasimishaji wa ajira, lipo kundi la madereva na makondakta wa daladala, ambao wamekuwa kwenye ajira kwa muda mrefu, lakini hawathaminiwi wala kupewa mikataba ili kuwafanya wawe na akiba kwenye mifuko ya hifadhi.

"Lini serikali itahakikisha ajira hii na yenyewe inakuwa rasmi na kutambuliwa kwa mujibu wa sheria?" alihoji.

Katika majibu yake, Mavunde alisema Waziri Jenista Mhagama amekwisha tekeleza agizo la Waziri Mkuu la kuwaita wamiliki wa vyombo mbalimbali vya moto na chama cha madereva ili kutengeneza mpango wa pamoja wa kurasimisha ajira za madereva. Alisema mpaka sasa, wanaendelea na ushirikiano na wamiliki wa vyombo hivyo.

"Tumepeana muda ili kufanya ukaguzi kubaini kama makubaliano yetu yamefikiwa ili madereva wote wa magari makubwa na madogo nchini wote wapate mikataba ya ajira kama sheria inavyoelekeza katika kifungu cha 14 cha sheria namba sita ya mwaka 2004,"alisema.

Katika swali la msingi, Mbunge wa Viti Maalum, Grace Tendega (Chadema), alisema wakati akiwaapisha wakuu wa mikoa Machi mwaka 2016, Rais John Magufuli alitoa agizo la kuwakamata vijana wote watakaokutwa wakicheza mchezo wa 'pool table' na kuwapeleka kambini wakalime.

"Serikali imeandaa kambi ngapi na kujua huduma za kujikimu kwa vijana hao wakati watakapokuwa wakiendelea na shughuli za kilimo na kipindi cha kusubiri mavuno yao?" alihoji.

Akimjibu mbunge huyo, Naibu Waziri Mavunde aliema serikali kupitia tawala za mikoa na wilaya imetenga maeneo maalum ya uzalishaji mali kwa vijana ambapo jumla ya ekari 217,882.36 zimeelekezwa katika kukidhi mahitaji ya shughuli za kilimo, ufugaji, viwanda na biashara ndogo.

"Kuwapo wa vituo vya maendeleo ya vijana na majengo ya viwanda kumesaidia kuwapa mafunzo vijana na kuwajengea uwezo wa kuongeza thamani katika mazao ya kilimo," alisema.

Aliongeza kuwa katika kukabiliana na tatizo la ukosefu wa ajira kwa vijana, serikali imeendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ikiwamo kuwajengea vijana ujuzi kupitia programu ya kukuza ujuzi nchini ili vijana kutumia ujuzi wa mafunzo mbalimbali kujiajiri na kuajiri vijana wengine.

"Katika mwaka huu wa fedha, serikali inatekeleza mafunzo ya stadi mbalimbali za kazi ambapo jumla ya vijana 49,265 watanufaika,"alisema.



Ofisa Masoko wa Jiji la Dodoma, James Yuna (kulia), akitoa maagizo kwa mzoa taka wa soko kuu la Majengo jijini humo jana, kuhusu uondoaji wa takataka zilizoingizwa na wafanyabiashara wa bidhaa mbalimbali kutoka mikoani, zilizopigwa marufuku kutupwa kwenye madampo ya masoko ya jiji hilo. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Wachunga mifugo jijini sasa kukiona

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

HALMASHAURI ya Jiji la Dodoma, imetangaza kuanza kuwachukulia hatua kali za kisheria wananchi ambao mifugo yao imekuwa ikila miti iliyopandwa jirani na maeneo yao.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Mkuu wa Idara ya Mazingira ya Jiji hilo, Dickson Kimaro, alipozungumza kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Binilith Mahenge, wakati wa upandaji miti uliofanywa jana na wafanyakazi wa Benki ya Posta nchini.

Kimaro alisema jiji hilo litaendelea kuwachukulia hatua kali za kisheria wananchi wenye mifugo katikati ya jiji kwa kuwa wamekuwa wakiruhusu mifugo kuchunga kwenye miti inayopandwa jirani na maeneo yao.


"Ndugu zangu wananchi wa jiji hili, kwa hili hatutanii, tutahakikisha tunaendelea kuwachukulia hatua kali za kisheria watu wanaolisha na kuharibu mazingira ndani ya jiji letu," alisema. Kimaro alisema katika vikao vyao, walikubaliana upandaji miti utashirikisha makundi ya watu mbalimbali ili kuboresha madhari ya jiji ambapo miti zaidi ya 1,500 itapandwa.

Alisema kuna baadhi ya wananchi wamekuwa wakiharibu miti na kuchafua mazingira kwa kulisha mifugo yao inayofugwa katikati ya jiji hilo.

Aliishukuru benki hiyo kuunga mkono juhudi za kuboresha mazingira na kuzitaka taasisi zingine kuunga mkono jitihada hizo. Ofisa Mtendaji Mkuu wa benki hiyo, Sabasaba Moshingi, alisema lengo lao ni kuunga mkono kampeni ya kulifanya jiji hilo kuwa la kijani.

Moshingi alisema benki hiyo katika kuunga mkono juhudi hizo, imetoa miche ya miti 500 ambayo itapandwa katika eneo la Mtaa wa Mlimwa West hadi Mtaa wa Swawa.

Alibainisha kuwa miti hiyo itapandwa kandokando ya pande zote mbili za barabara kuu ili kuboresha mazingira ya eneo hilo."Tunapenda kuwashirikisha ninyi wananchi wa mitaa hii kwa sababu ninyi ndiyo mtakuwa walinzi wakubwa wa miti hii isiharibiwe na itawasaidia ninyi kupata hewa safi," alisema.





Katibu Mkuu wa Chama cha Demokrasia Makini, Ameir Hassan Ameir (wa tatu kulia), akitoa tamko la viongozi wa vyama kumi vya siasa Tanzania la kupongeza mafanikio ya miaka tisa ya uongozi wa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein, wakati akizungumza na waandishi wa habari, mjini Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Shein ajivunia ushirikiano kati ya Zanzibar na Angola

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, amesema Zanzibar na Angola zina mambo mengi ya kushirikiana ambayo yanaweza kuleta mafanikio makubwa kwa pande zote mbili ikiwamo sekta ya utalii.

Katika mazungumzo yake na Ikulu Zanzibar na Balozi wa Angola nchini, Rais Shein alisema nchi hizo zina mambo mengi ya kujifunza namna ya kuendeleza na kuimarisha sekta ya utalii.

Alisema kwa Zanzibar sekta ya utalii ni nguzo kubwa ya uchumi ambayo imekuwa ikichangia asilimia 20 ya Pato la Taifa na asilimia 80 ya fedha za kigeni.

Alisema kutokana na Angola kupata mafanikio makubwa katika sekta ya mafuta na gesi asilia, ipo haja kwa Zanzibar na nchi hiyo kushirikiana katika kuhakikisha Zanzibar inapanua wigo kwa nchi hiyo ambayo ni ya pili kwa uzalishaji wa rasilimali hiyo barani Afrika ikitanguliwa na Nigeria.

Akieleza kuhusu ushirikiano katika sekta ya elimu, Dk. Shein alieleza kuwa ipo haja kwa pande mbili hizo kushirikiana katika sekta ya elimu hasa kupitia vyuo vya nchi hizo kikiwamo Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) katika lugha hasa Kireno.

Alisema ushirikiano huo utaimarisha sekta hiyo ya elimu, ikiwa ni pamoja na kubadilishana utaalamu na wataalamu hasa katika lugha ya Kireno ambayo itasaidia Zanzibar katika kuimarisha sekta ya utalii.

"Nitumie fursa hii kumpongeza Rais wa Angola, Joao Lourenco, kwa kazi nzuri anayofanya ya kuiongoza nchi hiyo kwa mafanikio makubwa ambapo hivi sasa uchumi wake unakuwa kwa asilimia 8.4.

"Hayo ni miongoni mwa mambo yaliopelekea ushindi wa kishindo wa kiongozi huyo pamoja na chama chake cha (The People's Movement for the Liberation of Angola) MPLA)," alipongeza.

Balozi wa Angola nchini Tanzania, Sandro Agostinho de Oliveira, alisema Angola iko tayari kushirikiana na Zanzibar katika sekta ya utalii na mafuta na gesi hasa ikizingatiwa kwamba Zanzibar imeanza kupata mafanikio na kutajika duniani kote katika sekta ya utalii.

Alisema Angola pia iko tayari kutoa nafasi za masomo kwa Zanzibar katika chuo chake kinachotoa mafunzo ya mafuta na gesi asilia ikiwa ni njia moja wapo ya kuendeleza ushirikiano wa kihistoria uliopo.

Balozi huyo alieleza juhudi zinazochukuliwa na nchi yake katika kupambana na rushwa na nchi yake na mchakato wa ushirikiano na Zanzibar katika kuendeleza sekta mbalimbali za maendeleo ikiwamo sekta ya utalii, elimu, mafuta na gesi asilia pamoja na kuendeleza utamaduni.

# Serikali yafafanua uzalishaji kiwanda

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WIZARA ya Biashara na Viwanda, imesema Kiwanda cha Makonyo kilichoko Pemba, kimefanyiwa ukarabati mkubwa na kuwa na uwezo wa kuzalisha bidhaa, yakiwamo mafuta ya mimea.

Naibu Waziri katika wizara hiyo, Hassan Khamis Hafidh, aliyasema hayo jana wakati wa kikao cha Baraza la Wawakilishi alipotoa ufafanuzi kuhusu maendeleo ya kiwanda hicho.

Alisema kiwanda hicho sasa kinazalisha mafuta ya Makonyo na mafuta ya mimea aina ya Arki kufuatia kufanyika kwa ukarabati mkubwa wa uzalishaji wa bidhaa.

"Tumefanikiwa kukifanyia ukarabati mkubwa Kiwanda cha Makonyo kilichoko Wawi, Pemba ambapo sasa kina uwezo wa kuzalisha mafuta ya mimea aina ya Arki," alisema. Naibu Waziri huyo alisema ukarabati huo umefanyika kwa ushirikiano mkubwa wa wawekezaji kutoka China ambao watakuwa wakinunua mafuta ya Makonyo na Mkaratusi.

Aliwataka wakulima kuongeza uzalishaji na kuuza Makonyo katika Shirika la Taifa la Biashara ili kukiwezesha kiwanda hicho kukidhi uzalishaji wa mafuta.

Alisema Shirika la Taifa la Biashara (ZSTC) limeongeza bei ya Makonyo kutoka Sh. 1,000 hadi Sh.1,500 kwa kilo.

# Mahakama Unguja na Pemba kukarabatiwa

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Katiba na Sheria, Khamis Juma Mwalimu, amesema serikali inakusudia kuzifanyia ukarabati mkubwa Mahakama zilizoko Unguja na Pemba ili kuboresha utendaji wake.

Aliyasema hayo jana katika kikao cha Baraza la Wawakilishi alipojibu swali la Mwakilishi wa Magogoni aliyetaka kujua lini Mahakama ya Konde iliyoko Pemba itafanyiwa ukarabati.

Mwalimu alikiri jengo la mahakama hiyo kuwa katika hali mbaya na juhudi za kuzifanyia ukarabati mahakama zilizoko vijijini zinafanywa hatua kwa hatua.

Alisema jengo la Mahakama Kuu Vuga tayari limefanyiwa ukarabati mkubwa na kurudisha hadhi na haiba yake sambamba na jengo la Mahakama la Chake Chake, Pemba.

Alisema majengo ya Mahakama ya Makunduchi Mkoa wa Kusini Unguja, Mfenesini na Mwera yamefanyiwa ukarabati ili huduma bora zipatikane.

"Tumeyafanyia ukarabati majengo ya mahakama yaliyopo mjini na vijijini ili yawe na nafasi ya kutosha kuwawezesha wananchi kusikiliza kesi na mashauri yao kwa nafasi," alisema.

Alizitaja juhudi nyingine zinazofanywa na serikali kuwa ni ujenzi wa jengo jipya la Mahakama Kuu huko Tunguu, nje kidogo ya Mji wa Unguja.

Alisema jengo hilo la Mahakama Kuu ya Zanzibar linatarajiwa kuwekwa jiwe la msingi na Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein katika kipindi cha maadhimisho ya wiki ya sheria nchini.

Alisema majengo mengi ya Mahakama Kuu zilizoko Zanzibar ni yale ambayo yamerithiwa kutoka utawala wa Kisultani, likiwamo jengo la Mahakama Kuu Vuga katika eneo la Mji Mkongwe na Chake Chake, Pemba.



**BEKA**

Soma UK.15

JUMAMOSI FEBRUARI 8, 2020

BT BURUDANI TELE



# BILA NOTI POTEA
## LULU DIVA HATAKI MIDUME CHAWA

Soma UK.14

## BASI SAWA



# AT kwa hili unajifagilia

MWANAMUZIKI mkongwe wa miondoko ya mduara, AT, amesema anajivunia kuwa mrefu kwa sababu wanawake wengi wanapenda umbo hilo na kwamba hata muigizaji Tausi amethibitisha hilo kwa kusema hataki mwanaume mfupi.

Akipiga stori na EATV, AT amesema urefu ulimletea madhara kwani alikuwa anajigonga kwenye mlango wa bibi yake ambao ulikuwa mfupi, ila hajawahi kukosa mpenzi kutokana na urefu wake.

"Hakuna shida ambayo nimeipata wakati narefuka kama kujigonga sana kichwani kwenye mlango wa bibi yangu ambao ulikuwa ni mfupi, ila kuhusu wanawake wanapenda sana wanaume warefu wenyewe wakikaa wanaongea kabisa kuwa mtu mrefu anawapendeza, kwa mfano Tausi amesema yeye ni mfupi hataki mwanaume mfupi, urefu ni dili" amesema AT.



# Roma ukisikia wivu ndo huo

RAPA mwenye mashairi yenye utata, Roma Mkatoliki, amesema huwa anapata wakati mgumu anapoenda kliniki na mke wake na kukutana na daktari anayefanya vipimo ni kijana mbichi.

Kupitia maelezo ambayo ameyaweka kwenye mtandao wa Twitter, Roma Mkatoliki ameandika anapata changamoto pale anapomkuta kijana kwenye sekta hiyo kwa sababu kuna wengine wanafanya makusudi kwenye vipimo.

"Zama hizi ukienda kwenye ofisi, taasisi, kampuni, mashirika na idara nyingi wengi wa watumishi utakaowakuta ni vijana, ni jambo zuri ila napata changamoto sana ninapompeleka mke wangu kliniki na kumkuta daktari anayemfanyia vipimo ni yanki tupo sawa au pengine nimemzidi umri" ameandika Roma.



# BILA NOTI POTEA
# LULU DIVA HATAKI MIDUME CHAWA

WEWE kama kidume lakini huna noti, basi usijisumbue kumnyemelea mrembo na mwanamuziki wa BongoFleva, Lulu Diva, kwani unaweza kuumbuliwa kweupee na kupata aibu ya mwaka.

Lulu Diva, ameanika kigezo cha mwanaume wa kuwa naye ni lazima awe na pesa na kama hana huyo atakuwa hana kigezo cha kuwa naye katika uhusiano wa kimapenzi.

"Hata ndani ya siku mbili tu nitamtambua kama sio sahihi, endapo atakuwa hanipi pesa, nitajua kwamba huyu sio mtu sahihi kwangu, lazima mwanaume aje na pesa nitakuwa naye vipi kama hana au hanisapoti kwenye maisha na kunihudumia kama mtoto wa kike, kama ana mapenzi ya kweli halafu pesa hana abaki nayo mwenyewe hayo mapenzi " amesema Lulu Diva.

Akaongeza kusema "Lakini pia nikikuona muongo, sio mwaminifu, nikiona akili zako hazijakomaa hatuwezi kuwa pamoja, bora hata awe anamtambua Mungu, busara, hekima kitakuwa kitu kizuri sana, bora ninyimwe vitu vyote ila nisinyimwe hekima"

## INSTA-TWITTER





**Rafiki** wa kweli ni mama na baba.
Hawa wengine wala usiwaamini maana binadamu wa sasa wana roho saba -**Profesa Jay.**



**Wahenga** wana mambo sana. Wanakwambia tenda wema nenda zako usingoje shukrani. Sababu baada ya kutenda wema, ni wachache sana wanakumbuka kama wametendewa. Wewe shukuru Mungu kwa kila jambo- **Rose Ndauka.**



## Nay wa Mitego unamtakia nini Ben Pol?

PENGINE anasubiri kutoa jibu sahihi! Lakini dongo la rapa Nay Wa Mitego ambaye alimwambia msanii mwenzake Ben Pol kwamba amepata ganda la ndizi hadi amejikuta akisahau muziki na kulelewa nchini Kenya, bado halijapatiwa jibu

Nay wa Mitego amesema hivyo kupitia wimbo wake wa ipo sawa, baada ya Ben Pol kula bata sana nje ya nchi akiwa na mpenzi wake Anerlisa Muigai.

Hata hivyo, Pol akijibu tuhuma hizo, amesema anatafakari lakini hana amejibu mazuri ya kumwambia Nay Wa Mitego.

"Huwezi amini kwenye bata nililokula sio kama kuna mtu nataka kumkomoa au kutaka kumuonyesha mtu kitu chochote ni ukurasa wa maisha ambao umepita au upo ninaouishi, cha umuhimu ni kwamba, hakuna dhuluma wala cha haramu au ushenzi wowote unaofanyika, kuhusu Nay wa Mitego mmmhh sina maneno mazuri kwenye hilo na sina cha kumwambia" ameeleza Ben Pol.




**>>> Usikose Jarida hili la Burudani Tele (BT) ndani ya Gazeti lako la Nipashe kila Jumamosi, pia lipo kwenye mtandao wa kijamii Twitter, tu' follow**

**@burudanitele**



# WAMBEA WAMLIZA BEKA FLAVOUR NAYE KAACHWA HIVIHIVI

STORI za kuachwa zinaendelea kuibuka kila siku, baada ya Stamina na Mabeste, sasa Beka Flavour, amekuja na mpya baada ya kudai kuachwa na mama watoto wake kutokana na umbea.

Beka Flavour amethibitisha hayo akisema kuna watu kazi yao ni kufuatilia maisha ya watu maarufu na wanapogundua hutaka kuanzisha stori.

"Ni kweli hatupo pamoja kwa sasa, sijafuata mkondo wa Aslay, watu wengi wameachana na mahusiano yao mengi tumeyafahamu kupitia mitandao ya kijamii, lakini yapo mengi ambayo hatuyafahamu hawajayaweka mitandaoni, hata mimi kwangu sikutaka watu wajue kama nimeachana na mama watoto wangu"

Akaongeza kumwaga mchele "Unajua sasa hivi kuna wambea, udaku na ufukunyuku mwingi na watu wapo kwa ajili ya kazi hiyo ni kufuatilia maisha ya watu maarufu, wakigundua wanataka kutengeneza stori na walijaribu kufanya hivyo japokuwa mimi sikuliweka hadharani ila sasa hivi limenifikia"

Beka Flavour na mpenzi wake huyo wamepata mtoto mmoja wa kiume aitwaye Aaryani ambaye ana umri wa mwaka mmoja na miezi minne.

## INSTA-TWITTER

Tuffolow/ Tu-tag
**@burudanitele**



**Kabla** ya kusema Tafakari. Vitendo vinaongea ukweli kuliko maneno- **Faiza Ally**.



**Ukitaka** kujua maadui zako subiri ufanikiwe-**Nandy.**



**Ufunguo** wa kufilisika na kutaka kujaribu kumridhisha kila mtu- **Roma Mkatoliki.**

# Kuumbe!



# BONGO KAWAIDA SANA
## KWA MEEK MILL, NICKI MINAJ INAWASUMBUA

KWA wasanii wa Bongo mabifu kati ya wasanii ambao wana uhusiano wa kimapenzi ni jambo la kawaida. Tunashuhudia jinsi wasanii hao wakitumia mitandao ya kijamii kuchafuana na kutupiana maneno ya ovyo.

Lakini huko Marekani mambo yamekuwa tofauti, mabifu kati ya msanii na msanii yanaweza kuleta hata maafa ikiwamo mauaji. Bifu linaloendelea hivi sasa ni kati ya Meek Mill na aliyekuwa mpenzi wake Nicki Minaj.

Wawili hao wameibua moto mpya baada ya kimya cha muda mrefu kiasi ambacho mtandao wa Twitter umekuwa moto kutokana na kurushiana maneno mazito.

Sakata la kurushiana maneno lilianza baada ya 'Like' ya Meek Mill kukutwa kwenye moja ya post ya mpenzi wa Nicki Minaj, Kenny Petty ambayo iliwekwa katika ukurasa wa Instagram na akaunti moja ya shabiki wa Nicki Minaj.

Posti hiyo ilimfikia Nicki na kuanza kumchana Meek Mill akimtaka aendelee na maisha yake.

Rapa huyo wa kike hakuishia hapo aliendelea kumrushia maneno Mill kwa kumwambia ananyanyasa wanawake kwa kuwapiga, akitoa ushahidi kwamba alishawahi kumpiga Dada yake huku akijirekodi.

Tuhuma za kupiga wanawake hazikuwa nzuri kwa Mill ambaye aliibuka na kutweet za Minaj ambapo akajitetea kwa kusema sifa ya kuwapiga wanawake ndiyo kitu pekee anakitumia kutaka kuharibu karia yake.

Mill akaenda mbali zaidi na kueleza jinsi Minaj pia alivyowahi kushiriki kulipa fedha kutaka kesi ya kaka yake kuhusu kubaka kutaka ifutwe.



# Wachekeshaji vijana wanaotamba Bongo

Na Adam Fungamwango

TAIFA la Tanzania kwa miaka ya karibuni limewapoteza baadhi ya waigizaji wa filamu za ucheshi kama King Majuto, Mzee Jongo, Pwagu, Kinyambe na wengineo wengi.

Ni waigizaji ambao waliliacha taifa likiwa kwenye simanzi na majonzi makubwa kwa kuwapoteza waigizaji hao waliowazoea, ambao walikuwa wakiwaliwaza pale wanapokuwa wamepumzika majumbani, baada ya kutoka kwenye shughuli zao za kujipatia riziki.

Hata hivyo, bado kuna baadhi ya waigizaji wakongwe ambao bado wamebakia kama mzee Pembe, Mzee Jangala, Kingwendu na wengineo ambao bado walisukuma gurudumu la sanaa hiyo ya uigizaji wa ucheshi.

Kwa miaka ya hivi karibuni, kumeibuka vijana wengi ambao wameingia kwenye sanaa hii ya filamu ya ucheshi, huku baadhi yao wakikonga nyoyo za mashabiki kwa kiasi kikubwa.

Leo tunawaangazia wasanii wa maigizo au filamu za ucheshi maarufu kama 'komediani', ambao kwa sasa wamejichukulia umaarufu nchini.

**Brother K**

Wakati mwingine hujitambulisha kama 'Tajiri wa Kigoma'. Ni mmoja wa wasanii vijana ambao wamekuja juu kama moto wa kifuu kwa sasa nchini. Wapo baadhi wanasema kuwa huyu ndiye mrithi halisi wa Mzee Majuto. Kwa sababu imefikia wakati siyo mpaka achekeshe ili watu wavunjike mbavu.

Akitokea tu, ukimuangalia, basi mbavu huna. Brother K, huigiza kwa lafudhi ya kabila la Waha wa Kigoma. Mbali na kuigiza kwenye moja ya televisheni binafsi hapa nchini, lakini pia amekuwa mara moja moja akionekana kwenye filamu, pia matangazo ya biashara.

Aina yake ya ucheshi, anavyotamka maneno yake, vituko, pamoja na mavazi yake, hasa uvaaji wa shati kubwa linalokaribia kuwa kama kanzu au dera, linamfanya kujipambanua na kuwa mmoja wa waigizaji wa kipekee hapa nchini.

**Kipupwe**

Huyu ni mmoja wa waigizaji makomediani vijana kabisa wanaoinukia kwa kasi hapa nchini.

Huonekana kwenye filamu mbalimbali ambazo huzicheza yeye na wenzake na kusababisha burudani ya aina yake kwa watazamaji, kutokana na ucheshi na maneno yao ya kuguezageuza maana.

**Tin White**

Ni mmoja waigizaji vijana wanaochipukia kwa kasi na kuzidi kujipatia umaarufu hapa nchini.

Ingawa bado hajafika kwenye levo za kina Majuto, au Jangala, lakini kama akijitahidi kutokana na umri wake bado umamruhusu anaweza kabisa kufika huko.

Kutokana aina yake ya uigizaji, hata baadhi ya wasanii wa bongo fleva wamekuwa wakimchukua ili kupambana video zao kwenye baadhi ya matukio yanayohitaji ucheshi na hasa wale wa muziki wa singeli.

**Mau Fundi**

Huyu yupo kundi moja na Kipupwe. Wamekuwa wakiigiza wote kwenye filamu mbalimbali, kiasi kwamba kama filamu ambayo mmoja wapo hayupo ni kama kuna utamu filani hivi unakosekana.

Ni mwigizaji anayeongea kwa upole, lakini maneno yake yamekuwa yakifurahisha, huku pia akizungumza kwa staili ya 'kithethe'.

**Kiwewe**

Ni msanii kijana ambaye hadi leo bado hajachuja kwenye tasnia hii ya filamu za ucheshi. Ameendelea kuwa kwenye kiwango kile kile tofauti na baadhi ya wasanii tena vijana kama yeye na alianza nao ambao kwa sasa ni kama viwango vyao vimeporomoka.

Kiwewe ameendelea kubaki kwenye kiwango kutokana na kukubali kubadilika kutokana na mazingira ya kazi yenyewe inavyotaka, pamoja na uhitaji wa mashabiki wake.



# IMETOKEA

## Pombe yatoka kwenye mabomba badala ya maji

WAKAZI wa mtaa mmoja wa nyumba za ghorofa kusini mwa India walipigwa na butwaa baada ya mchanganyiko wa pombe kuanza kutoka katika mifereji yao.

Mchanganyiko huo wa rangi ya kahawia ulianza kutoka kwenye mifereji ya jikoni katika nyumba hizo jimbo la Kerala siku ya Jumatatu asubuhi.

Wakazi hao hawakufurahishwa na kisa hicho, waliamua waliwasiliana na mamlaka husika ili kupata msaada na kugundua kwamba kisima cha maji kilichafuliwa na maofisa kwa bahati mbaya.

Ilibainika kwamba lita 6,000 za pombe zilikuwa zimezikwa karibu na eneo hilo.

Pombe hiyo ambayo maofisa walikuwa wameiweka katika shimo baada ya kuchukuliwa kutokana na agizo la mahakama ilipenya mchangani kabla ya kuingia katika kisima hicho ambacho ndio chanzo cha maji yanayosambazwa katika ghorofa 18 za wilaya ya Thessur.

"Tulishangaa", mmiliki wa ghrofa hizo alimuambia mwandishi wa BBC Hindi Imran Qureshi.

Kwa bahati nzuri harufu kali iliokuwa ikitoka katika mifereji hiyo haikuwavutia watu hao .

Hatahivyo ugunduzi huo ulisababisha kukosa maji ya kunywa kwa familia na pia hawakuweza kuosha vyombo vyao.

"Watoto hawakuweza kwenda shule na hata wazazi wao hawakuweza kwenda kazini", alisema bwana Malyiekkal.

Baada ya malalamiko hayo, maofisa waliingilia kati ili kurekebisha makosa. Hatahivyo huenda ikachukua muda wa mwezi mmoja kusafisha kisima hicho ,kulingana na taarifa.

"Wamekuwa wakisambaza takriban lita 5000 za maji kila siku lakini hazitoshi kuhudumia familia zote katika nyumba hizo", alisema Malyiekkal akiongezea kwamba kisima hicho ndicho kilichokuwa chanzo pekee cha maji,

Maofisa kutoka kwa idara hawakuweza kutoa majibu sahihi kwa BBC.

Jimbo la Kerala lina sifa ya unywaji mkubwa wa pombe nchini humo





## Ndoa Talaka
## Mapenzi hayachezewi kama mdoli

**Na Adam Fungamwango**

DHULUMA yoyote ile ni kitu kibaya. Tamaa nayo vile vile si nzuri katika ustawi wa jamii. Leo nitazungumzia dhuluma ya mapenzi. Usicheze na moyo wa mtu.

Kuna baadhi ya watu wanawarubuni wenzao kuwa wanawapenda. Na wenzao wanapokubali na kuamua kuwapa moyo na mapenzi yao yote wakitumaini kuwa wanapendwa, wanakuja kuwabadilishia kibao. Kumbe hayakuwa mapenzi ya kweli, ilikuwa ni kucheza na moyo wa mtu.

Hili ni jambo baya sana na kwa sasa limekuwa sugu kwenye jamii. Na hii yote inatokana na sababu mbalimbali ikiwamo tamaa.

Mkasa huu umo kwenye filamu ya 'Ndoa Talaka', ambao unaifundisha jamii kutocheza na hisia za mtu.

Kipupwe ana mchumba wake ambaye ni Hadija. Huyu ni mchumba wa siku nyingi kwa miaka minne na tayari walikuwa wameshapanga kuoana.

Kila mmoja kijijini alijua fika kuwa Kipupwe atamuoa Hadija. Lakini siku isiyo na jina Kipupwe alitangaza ndoa.

Kijiji chote kilifurahi kwa kudhani kuwa atamuoa mchumba wake wa siku nyingi Hadija. Haikuwa hivyo. Aliyetangazwa ni Fatuma. Binti anayetoka kwenye familia ya kitajiri.

Watu walihamanika, lakini hakuna aliyeweza kugeuza ridhaa ya mtu. Kipupwe ndiye muoaji. Haikuwezekana kumpangia mtu atakayemuoa.

Wakawa wanatazama tu kwa macho. Hadija na Fatuma wanafahamiana. Na mara kwa mara wanakutana. Kitendo cha kukutana mara kwa mara kinamuweka kwenye wakati mgumu Kipupwe kwa sababu hajui nini wanachoongea.

Mara nyingi, au kwenye hali ya kawaida ilibidi wagombane kwa sababu wamechukuliana. Lakini sivyo.

Alichofanya Hadija ni kwenda tu nyumbani kwa Kipupwe na kumuuliza ni kwa nini amemgeuka, kwani amemuweka miaka yote minne akiwakataa wanaume wengi kwa ajili yake, lakini leo anamtosa?

Kipupwe anamtuliza na kumwambia kuwa asiwe na wasiwasi kwani anachofanya ni kumdanganya tu Fatuma, alichofuata kwake ni mali tu na anachofanya ni kumuoa, halafu akishazidhibiti mali, anampa talaka na kuja kumuoa yeye Hadija. Ni jibu ambalo halikumridhisha Hadija.

Siku za harusi zilikaribia. Hadija na shoga zake walishona sare kwa ajili ya mwenzao, Bi. Harusi Fatuma. Siku ikawadia. Sherehe ikafanywa. Harusi ikafungwa. Wakati wa kugawa zawadi, Hadija alikwenda kwa Fatuma na kumwambia kuwa huyo aliyenaye ni mchumba wake na anamuomba amuachie, lakini pia akamwambia kuwa wao wanapendana sana, lakini Kipupwe ameamua kumuoa kwa sababu ya kufuata mali tu zilizopo kwenye familia yao na si kwa sababu ya mapenzi.

Maneno hayo yanachoma Fatuma. Wakiwa bado juu jukwaani, anamuuliza yale yote yaliyosemwa ni kweli? Kipupwe anajiuauma katika majibu yake. Bi. Harusi anaamua kumuomba talaka hapo hapo kwa sababu amegundua kusudio la harusi hiyo.

Ni harusi ambayo imefungwa muda huo huo na Bi. harusi kudai talaka kwa muda usipungua dakika 10 hivi.



# BARUA YA WAZI KWA OPRAH ATAJWA MBINAFSI, MBAGUZI

MWIGIZAJI nyota wa Marekani, Mo'nique ameamua kupasua jipu baada ya kumwita mwendeshaji wa vipindi vya majadiliano, Oprah Winfrey kuwa ni mbinafsi na asiyewaunga mkono watu weusi.

Katika waraka mrefu aliouweka katika ukurasa wake wa Instagram, mwigizaji huyo mshindi wa tuzo mbalimbali amesema aligundua tabia hiyo siku za hivi karibuni, baada ya kukaa kimya katika matukio ya watu weusi kubaguliwa.

"Ndugu Oprah, nilihisi kulazimika kukuandikia barua hii wazi baada ya kuona utofauti kwa njia ambayo unaonekana kwa watu ambao walituhumiwa ubaguzi".

Ulifanya mahojiano kwenye kipindi cha CBS Morning na uliulizwa kuhusu Harvey Weinstein na Norah O'Donnell, umesema kama inajilinda binafsi, ilijibu eti kila wakati unajaribu kutazama upinde wa mvua kwenye mawingu. Pia ulisema ikiwa utafanya haya yote kuhusu Harvey Weinstein basi tumepoteza wakati huu," Kulingana na mwigizaji huyo kuwa majibu hayo yalionesha kwamba kujitenga nao, jambo ambalo yeye kama Mmarekani mweusi hapaswi kufanya.

Akaongeza "Wakati wewe ungetaka kuwa sehemu ya maandishi ya Michael Jackson na Russell Simmons, ni jinsi gani hiyo haifanyi yote juu yao? Alihoji.

Alizidi kuhoji kwamba jambo la kufurahisha MJ aliachiliwa huru, na kisha amekufa, kwa hivyo ni vipi hajazuiliwa ?

Amesema Russell na Harvey wanatuhumiwa kwa makosa kama ya Jackson kwa nini hawasaidii.

Katika kukazia hoja yake, Monique amesema anakumbuka wakati alipokuwa na harakati ya kukuza mradi wake miaka michache iliyopita, Oprah alikataa kutoka nje kuzungumza naye.

"Uzoefu wangu binafsi, wewe umenitazama kama mwanamke mweusi" Akazidi kumimina tuhuma hizo kwa Oprah "Wakati nilikuwa na miaka kumi na sita na nikakutana na wewe kwenye onyesho lako la ndani huko Baltimore, nilikuambia nataka kuwa kama wewe, ulinijibu lazima ufanye kazi kwa bidii sana,"

"Binafsi sikujua kuwa wewe ukimya wako unakosa kufanya maovu, ungefanya maisha yangu kuwa magumu," akasisitiza katika barua hiyo.

Mwisho alimshauri kufikiria kusimama na watu ambao ni sawa na sio watu sahihi tu.

# Kidjo,Yemi waangusha 'Shekere' hadharani



MWANAMUZIKI mkongwe barani Afrika, Angelique Kidjo akishirkiana na Yemi Alade, wametambulisha kibao chao kipya kinachoitwa 'Shekere' ambacho video yake imefanyika Afrika Mashariki.

Wimbo huo wenye maadhi mchanganyiko wa Calypso na Kwaito ni marudio ya wimbo wake ambao umempatia tuzo ya Grammy mwaka huu 'Mama Africa'.

Pia wimbo huo unaendana na wimbo wake mwingine 'Wombo Lombo' ambao Kidjo anajivunia nao kwa muda mrefu.



## Kweli Lil Wayne wewe Mnigeria?

RAPA maarufu wa Marekani, Lil Wayne, amesema ana asilimia 53 kuwa na asili ya Nigeria.

Nyota huyo wa muziki amesema hayo wakati akifanya mahojiano na marapa wenzake N.O.R.E. na DJ EFN ambao wanaendesha kipindi cha 'Drink Champ show' kwenye televisheni ya Revolt TV.

"Nasema kwa nguvu kwamba nina asilimia 53 mimi Mnigeria,ndiyo mimi na mama tunahitaji kusema hivyo," amesema Lil Wayne.


## Paul Okoye atishia nyau

MWANAMUZIKI PAUL Okoye, ametishia kukabiliana na Tume ya hakimiliki ya Nigeria kwa madai ya kudhulumu haki za wasanii.

Paul Okoye, ameiita Tume hiyo kuwa ya kitapeli na kwamba ataichukulia hatua kali kwa kudhulumu haki yake.

Msanii huyo wa kundi lilovunjika la Psquare, ametumia ukurasa wake wa Instagram kusema "Sijawahi kujua Tume ya hakimiliki ya Nigeria ni wateka nyara, wanaweza kumtia kizuizini na kuuliza dhamana ... Mpendwa NCC nimekaribia kuwamaliza yinyi," ameandika.





## Seun Kuti awabwatukia polisi

MWANAMUZIKI wa Afrobeat kutoka Nigeria, Seun Kuti, amekasirishwa na kitendo cha kuzuia bodaboda kupakia abiria katika maeneo ya miji.

Mshindi huyo wa tuzo mbalimbali, ametumia ukurasa wake wa Instagram kueleza utumiaji wa chombo hicho katika usafiri wa umma unahitajika.

"Wanigeria wenye taaluma lazima waoneshe hali halisi tunayoisubiri, watoto wanakimbizwa hospitali kila siku bila kujalisha aina ya chombo kuwahishwa matibabu. Police wanazuia basi watuambie kama mabasi yanaweza kutufikisha kazini kwa muda sahihi," amehoji Kuti.

## Chris Brown kwa hili mmh!

MWIMBAJI wa Marekani, Chris Brown, amejikuta akiibua mjadala katika mitandao ya kijamii baada ya kushiriki picha inayomuonesha mzazi mwenzake, Ammika Harris, akimbeba mtoto huku akiwa hana nguo ya juu.

Picha hiyo ambayo imewashangaza watu wengi, inamuonesha mrembo huyo akimbeba mtoto wake Aeko, kifuani bila kuwa na nguo.

Baadhi ya mashabiki wake wameonekana kuipenda picha hiyo, na wengine wakilalamika haina heshima kwa jamii.





**MIONZI YA SHERIA**

# Taratibu za kulipwa gharama za shauri au kesi

Na John Juma
0716217615

KUNA tofauti kati ya gharama za shauri/ kesi (costs), fidia (compesation) na faini(fine). Gharama za shauri/kesi, zenyewe, ni nje ya vyote tangulia kusema hapo juu. Lakini pia ni nje ya kile ulichoshindambebwa na hukumu. Kimsingi, kufuatia amri alipwe fidia au amri alipwe faini haimaanishi gharama husika zimesha jumuishwa/kuhesabika humohumo. Laa hasha, pamoja na fidia, kadhalika mhusika atastahiki vilevile na gharama ambazo moja kwa moja zimetokana na shauri/ kesi husika.

Ukweli ni kuwa watu wengi huwa hawadai gharama za shauri/kesi. Mtu akishaambiwa ameshinda tu basi, mengine hataki kujua/kusikia. Kama imeamriwa alipwe pesa, au kama ni mali kama ardhi imeamriwa arudishiwe, au ushindi mwingine wowote basi huondoka tu moja kwa moja bila kudai gharama zake. Sasa yafaaniwajuze kuwa nje ya ushindi utokanao na kubebwa hukumu; bado tena unayo haki ya kudai kulipwa gharama zote ilizotumia katika za kuendeshea shauri/ kesi hsika.

GharamazaShauri/Kesi hujumuishanini/zikoje?

Gharama za shauri/kesi ni yale matumizi yote halali uliyoingia wakati ukishughulikia shauri/kesi husika. Hizi ni pamoja na nauli ulizokuwa ukitumia kutoka nyumbani kwenda Mahakamani kwa kipindi chote cha shauri/kesi mpaka kufikia tamati yake, pesa uliyomlipa Wakili kama ulikuwa unawakilishwa na Wakili, pesa uliyotumia kumlipa Wakili kuandaa nyaraka, pesa ya kuchapa(print),pesa ya kutoa vivuli (kopi)vya/za nyaraka mbalimbali ulizokuwa ukiwasilisha Mahakamani, na gharama nyingine yoyote ambayo uliingia wakati ukifuatilia kesi/shauri.

Isipokuwa tu gharama tajwa ziwe ni zile ambazo ni halali kwa asilimia mia moja (100%). Rushwa na gharama nyingine za kutengeneza ambazo, kwa kujua au kutokujua, katu hazikubaliki kulipwa: kwani ni kosa kufanya hivyo.

**YUPI/AKINA NANI HUTAKIWA KULIPA GHARAMA ZA SHAURI/KESI?**

Aliyeshindwa (mwangushwa na hukumu) hutakiwa kumlipa aliyeshinda (mbebwa na hukumu). Mfumo unaofuatwa na Nchi za Jumuiya ya Madola (Common law) hakuna utaratibu wa kila mtu/upande kushinda katika shauri/kesi, lazima mmoja ashindwe (no win-win situation). Yaani, mfumo wa shinda-shindwa(win-loose situation).

Hivyo basi, yule aliyetangazwa kushindwa anawajibika kumlipa gharama aliyeshinda. Na haijalishi iwapo huyo aliyeshinda alikuwa mlalamikaji/mshitaki, au alikuwa mlalamikiwa/mshitakiwa. Muhimu ni kwamba ameshinda, atalipwa gharama zake.

**AMRI YA KULIPA GHARAMA**

Hakimu au jaji aliyekuwa anasikiliza shauri/kesi husika ndiyo anayetoa amri husika. Isipokuwa mlalamikaji au mlalamikiwa (kulingana ni yupi hukumu imembeba) anatakiwa kuomba gharama hizo, kama jinsi ilivyotangulia kueleza hapo awali. Halikadhalika, wakati muafaka kwa/wa kuomba kulipwa gharama ni wakati ule ule ambapo shauri/ kesi ikiendelea kusikilizwa.

Gharama, kwa kawaida, hazitolewi moja kwa moja, hivyo tena nasisitiza ni muhimu kuziomba. Na wakati wa kuziomba ni huo huo, wakati shauri/kesi inaendelea.

Umuhimu (Uzito) wa Ushahidi

Ni muhimu sana wakati shauri/kesi inaendelea na mhusika ameshawahi kisha ombi tajwa, ziwepo tayari risiti ya kila gharama ambazo mhusika anadai kuingia. Hata kama fedha kufuatia kutoavivuli/kopiza nakala/nyaraka ni muhimu kuwahi na stakabadhi/risiti ya huduma hiyo/ hizo toka kwa mtoa huduma; itasaidia sana Mahakama kujiridhisha kabla ya kufikia uamuzi tarajiwa. Kwani, gharama ambayo/zo mhusika hatakuwa na uthibitisho nazoa(stakabadhi/risiti) ipo hatari/uwezekano mkubwa wa zenyewe kukataliwa.

Hii husaidia pia kutotumia nafasi hiyo kumkomoa mtu ili alipe zaidi hata kwa kile ambacho hukutumia.

Kwahiyo unashauriwa tangu siku ya kwanza unapopokea wito wa kuitwa Mahakamani, au siku ya kwanza kufungua shauri/kesi, hakikisha kila hatua yako unakuwa na risiti ili iwe rahisi kulipwa gharama zako.

**MUDA/WAKATI GHARAMA HULIPWA/ZITALIPWA**

Kama ilivyotangulia kugusiwa hapo awali, kidogo. Gharama tajwa hulipwa mwishoni kabisa, baada yashauri/kesi kuisha. Gharama haziwezi kulipwa kabla, kwasababu kabla ya hapo ni vigumu kwa mhusika kujuaatatumia fedhakiasi gani. Yaani, ni ngumu kufanya majumuisho ya gharama kwa kina.

Kimsingi, gharama zitalipwa mwishoni kwakuwa hapo ndipo unapoweza kufanya majumuisho kuanzia mwanzo washauri/kesi lilipoanza hadi mwisho lilipoisha na kujua kwa kina umetumia kiasi gani.

Mwisho, ni vema sasa tufahamu kuwa nje ya kushinda na kuambiwa ulipwe fidia, urudishiwe nyumba/kiwanja, au ushindi mwingine wowote; bado ipo haki kwa kila mhusika kuomba kulipwa gharama ambazo ameingia/ataingia katika kushitaki au kujitetea. Hii ni kulingana na ipi hasa nafasi yake katika shauri/kesi yenyewe. Naomba kuwasilisha!

# Fahamu mambo muhimu kuhusu Corona

Na mwandishi wetu

MAMLAKA ya afya nchini China inajaribu kila njia kuudhibiti mlipuko wa virusi vya Corona ambavyo vimesambaa kote duniani tangu kuripotiwa kwake.

Chimbuko la ugonjwa huo ni mji wa katikati wa Wuhan kulingana na gazeti la South China Morning post.

Wakati huohuo, maofisa wanakabiliana na uvumi kuhusu elimu potofu kuhusu mlipuko huo.

Na hizi ni baadhi ya mambo yanayoleta utata kuhusu Corona.

Je virusi vinaweza kusambazwa kwa mtu mmoja hadi mwengine?

Mtaalam wa ugonjwa wa Sars nchini China, Zhong Nanshan, alithibitisha kwamba usambazaji wa virusi hivyo kutoka mtu mmoja hadi mwengine unaweza kufanyika.

Hii inatokana na tume ya afya mjini Wuhan kusema hapo awali kwamba hakuna uthibitisho wa usambazaji wa virusi hivyo kutoka kwa mtu mmoja hadi mwengine.

Uthibitisho kuwa ugonjwa huo unaweza kusambazwa kutoka kwa mtu mmoja hadi mwengine imeungwa mkono na tafiti za kimatibabu ikiwamo moja iliochapishwa katika jarida la afya duniani la Lancet.

**JE KUNA TIBA YOYOTE YA UGONJWA HUO?**

Wanasayansi hawajapata tiba sahihi ya ugonjwa huo uliobainika hivi karibuni, ambao unaweza kusababababisha dalili nyingi miongoni mwa wagonjwa, ikiwamo kuharisha.

Vifo vingi kufikia sasa vimewakumba watu wenye magonjwa mengine kama vile kisukari , lakini mwathiriwa mwenye umri mdogo kabisa ni mtoto wa siku tatu.

Tume ya afya mjini Beijing awali ilikuwa imesema kwamba itatumia dawa za kukabiliana na virusi vya ukimwi kama mojawapo ya tiba zake za virusi hivyo vya Corona.

Afisa mmoja anayefanya kazi na taasisi ya kitaifa ya afya wiki iliopita alisema kwamba shirika hilo lilikuwa linatengeneza chanjo ya virusi vya Corona ambayo huenda ikaanza kufanyiwa majaribio miongoni mwa wanadamu katika kipindi cha miezi mitatu ijayo.

Je dawa za kitamaduni hutibu virusi vya Corona?

Machapisho ya mitandao ya kijamii yamesema kwamba tiba za kiasili kama vile kugogomoa maji ya chumvi na kula karafuu iliochanganywa na vitunguu thaumu kunaweza kutibu virusi hivyo.

Hatahivyo tume ya kitaifa ya afya wiki iliopita ilipinga uvumi kwamba unywaji wa mchangayiko wa siki na


**JE KUZIBA PUA KUNAWEZA KULINDA DHIDI YA VIRUSI HIVYO?**

Kujiziba pua kumekuwa kitu cha kawaida nchini China na Hong Kong baada ya visa vya ugonjwa wa virusi vya Corona kuongezeka katika kipindi cha wiki moja iliopita

Huku idadi ya vitambaa vinazotumika kujiziba pua zikiisha katika maduka mbali na mitandaoni kote nchini humo, watengenezaji wake wameshindwa kukabiliana na mahitaji yake.

Vifaa hivyo vinaweza kumsaidia anayevitumia kujiziba pua kutosambaza virusi hivyo kupitia mdomo na pua. Lakini uwepo wa mwanya kati ya anayevaa na kifaa hicho ni thibitisho kwamba kuna hatari kubwa ya kupata ugonjwa huo.

Wataalam wa kimatibabu ikiwamo shirika la afya duniani WHO wamependekeza hatua nyengine za kujilinda kama vile kuosha mikono mara kwa mara, kuziba mdomo wakati unapokohoa, kupiga chafya na kuzuia ulaji wa bidhaa za nyama ambazo hazijaiva.



Kirusi cha Corona kinavyoonekana

**JE UCHUNGUZI WA VIWANGO VYA JOTO KUNAZUIA USAMBAAJI?**

Imethibitishwa kwamba wagonjwa wa virusi hivyo wanaweza kutoonyesha dalili za ugonjwa huo aina ya Pneumonia , lakini bado wanaweza kusambaza ugonjwa huo bila ya wao kuonyesha dalili kwa kipindi cha siku 14 ama wiki mbili.

Kulingana na David Heymann ambaye ni daktari wa magonjwa ya zinaa katika chuo kikuu cha London, kuhusu usafi na dawa za kitropikali, uchunguzi wa kiwango cha joto katika mipaka sio asilimia 100 kwa kuwa watu wanaweza kupita vipimo vya joto bila kuonyesha dalili zozote.

Kitu muhimu na mipaka ni kuwaelezea watu mahala pa kwenda iwapo vipimo vya vya joto vipo juu, uchungu kooni ama kupumua kwa matatizo.

Je imethibitishwa virusi hivyo vinatoka kwa wanyama?

Tume ya kitaifa ya afya nchini China, ilisema sampuli 33 zilizochukuliwa kutoka katika soko hilo la Huanan, mjini Wuhan vilithibitisha kuwepo kwa virusi hivyo.

Virusi hivyo hususan vilipatikana katika vibanda vya kuuza nyama , ambavyo vinauza wanyama wa mwituni.

Wataalam hawajabaini ni spishi gani ya wanyama walioasababisha maambukizi kwa binadamu , lakini tafiti mbili zinasema kwamba kuna uwezekano mkubwa kwamba vinatoka kutoka kwa popo ambao ndio chanzo cha virusi hivyo.

Hatahivyo , ripoti iliochapishwa katika jarida la Lancet inatoa changamoto ya maoni yanayolaumu mlipuko huo kutoka kwa soko hilo la vyakula vya baharini.

# Vijana wataka ajira zenye staha

## ■ Mabinti wachoshwa kuvaa nusu uchi, kukatazwa kuzaa, ajira bila mkataba

Na Gaudensia Mngumi

UKIFIKA katika maeneo ya viwanda kwenye miji mikuu unakutana na makundi makubwa ya vijana wanawake kwa wanaume, wanaojipanga nje ya malango ya kuingia viwandani wakiulizia kazi.

Mathalani, jijini Dar es Salaam, mamia ya vijana wanaojihimu kuwazidi wamiliki, wanakusanyika kwenye sehemu au ukanda wa viwanda kama Mbezi Beach, Tabata, Mikocheni, Nyerere Road na Vingunguti.

Sura za vijana hao wanaojihimu alfajiri kwenye mageti na uzio (fensi) za viwanda, zinaonyesha kukata tamaa, umaskini na utayari pamoja na uhiari wa kufanya kazi yoyote bila kujali hali, maslahi wala heshima anayostahili mfanyakazi.

Umaskini huo pamoja na utandawazi ndiyo unaowatumbukiza wengi kwenye kufanyakazi zisizo na staha, hazina mikataba, zisizoheshimu haki za watumishi, kama likizo, zenye malipo duni na zilizojaa unyanyasaji na changamoto mbalimbali ambazo huathiri zaidi wanawake.

Kujadili changamoto hizo, vijana wadau wa masuala mbalimbali ya maendeleo walikutana Dar es Salaam, mwishoni mwa Desemba kuangazia suala ajira zisizo staha na athari zake na kutoa mapendekezo yao.

Vijana kutoka Zanzibar na mikoa mingine ya Bara wanapozungumzia kazi za kidhalilishaji zisizo na staha wanasema, wasichana kunyonywa na kudhalilishwa sehemu za kazi hasa kwenye sekta ya utalii ni jambo linalohitaji kutupiwa macho.

Wanasema mabinti wanalazimishwa kuvaa mavazi mafupi, yanayoonyesha miili yao hasa matiti na tumbo ili kuwavutia wateja wa 'kasino' au hotelini.

Hoja hizo zinaibuka wakati wa mkutano wa kitaifa wa vijana uliooshirikisha wadau wengine kama idara za kazi na ajira, wabunge, asasi za kirai, wanahabari na wafanyakazi, unaofanyika Dar es Salaam, kujadili umuhimu wa taifa kuwa na mpango wa nchi wa kuwa na ajira zenye staha, uelewano na zinazoheshimu utu wa mtumishi.

Vijana kutoka Bara na Visiwani wanaowasilisha taarifa mbalimbali kuhusu kazi duni nchini, wanaeleza kuwa hotelini kumekithiri unyanyasaji mabinti na kwamba ni jambo la kawaida iwe migahawani, kwenye 'resort' ufukweni nguo za kudhalilisha ni kawaida.

Wanasema pale binti anapokataa kuvaa mavazi yasiyo na heshima, anatishiwa kwa kauli kali mfano, unataka kazi au unaleta ubishi? Jiangalie wenzako wanatamani kuwa hapa.

"Wakati mwingine wanalazimishwa kuvaa mavazi yanayoonyesha miili yao na kujipitisha kwa wateja hasa wanaume bila kujali kuwa wanadhalilishwa na wengine hulazimishwa kuwa ni lazima watumika kingono hata bila ridhaa zao ili kulinda heshima ya hoteli na wateja.

Vijana kutoka Zanzibar wanataja suala la kukosa mikataba yenye bima, matibabu, mafao kwenye mifuko ya akiba ya wafanyakazi kuwa ni changamoto zinazowatesa wafanyakazi wengine nchini kutokana na ajira zisizo na staha.



### MIKATABA MIAKA 100

Katika mkutano huo unaoandaliwa na Shirika la Kimataifa la Actionaid, linalofanyakazi na jamii kuinua maisha ya wanawake na vijana, washiriki wanaelezwa kuwa licha sekta ya utalii na uvuvi kuwa kinara wa muhimili wa uchumi wa Zanzibar, baadhi ya vijana wanakosoa jinsi baadhi ya waajiri wa sekta hiyo walivyo wanyanyasaji.

"Kampuni inapoajiri wavuvi na wafanyakazi hotelini wanasainishwa mkataba wa miaka 100. Lengo ni kuwabana na kuwadhulumu wafanyakazi hao ambao wanatakiwa kulipa gharama zote na kumfidia mwajiri iwapo watavunja mkataba huo. Hii ni ajabu." Anasema mwakilishi kutoka asasi ya Youth Coalition Zanzibar, Amina Bakari Yusufu.

Lakini si hivyo tu, anaongeza kuwa pamoja na mkataba huo, wapo waajiri wanaowasainisha wafanyakazi mikataba bila kuwapa nakala na wanapoondoka nayo hubadilisha baadhi ya vipengele na kuwa na mkataba unaombana mtumishi.

### SUALA LA UZAZI

Washiriki hao wanasema suala la uzazi linapigwa vita na waajiri na mara nyingi wasichana wanaobeba mimba wanahatari ya kukosa kazi na hata wakijifungua hawana likizo ya uzazi, hawaruhisiwi kurudi nyumbani kunyonyesha na kwa ujumla yote hayo husababisha watoto kukosa maziwa ya mama na kuwa na afya mbaya.

Wanasema ujauzito japo unakubalika kisheria na ni moja ya haki ya msingi ya mwanamke, waajiri wengi hawathamini uzazi na wanaona kama ni mzigo kuajiri wanawake wakihofia kuwa watabeba mimba na kuchelewesha au kurudisha kazi nyuma.

Baadhi ya wafanyakazi vibarua wa viwanda mbalimbali jijini Dar es Salaam, wanaozungumza na Nipashe katika mahojiano, wanasema changamoto hiyo ni kubwa na baadhi yao wanalazimika kufanyakazi hadi wiki ya mwisho wanapokaribia kujifungua.

Aidha, wanaongeza kuwa hata wanapojifungua wanaomba ruhusu ya siku saba na kulazimika kurudi kazini siku chache baada ya uzazi ili kuepuka kukosa kazi ambayo hata hivyo haina mkataba.

Kadhalika wanasema wakati mwingine ni lazima kutumia, fedha au hata rushwa ya ngono ili kuhifadhi nafasi za kazi kwani kama haujulikani au mambo yako hayaendani na kile msimamizi wako anachotaka kuna uwezekano wa kupoteza kazi.

Athari za utaratibu huo walidai ni kudhoofisha afya za wazazi ambao huwa dhaifu na watoto ambao serikali inaagiza wanyonyeshwe miezi sita bila kulishwa chochote.

Kwenye baadhi ya viwanda vya nguo wafanyakazi wanaeleza kuathirika kutokana na kushika kemikali za kutengeneza nguo kazi inayofanywa bila kuwa na vitendea kazi muhimu kama glovu.

"Tumechubuka mikono, ina majeraha makubwa ambayo hayatibiki kutokana na `salphuriki asid' inayotumiwa kutengeneza nguo. Tunakata majora tunashika nguo hizo ambazo bado zina tindikiali hiyo inayoumiza mikono," anasema mfanyakazi mmoja jina na kiwanda vinahifadhiwa , akiongeza kuwa katika mikataba yao hawana kipengele cha kuwapa vitendea kazi.

### KODI KIPAUMBELE...?

Vijana hawa wanaiona serikali inawabana waajiri wasiolipa kodi lakini haijaonyesha ukali kwa waajiri wasiothamini wafanyakazi, wasiojali mikataba, haki wala stahiki.

Serikali inakosolewa kwa kuwaadhibu waajiri wasiolipa kodi, tozo na stahiki nyingine lakini haishughuliki kikamilifu na waajiri wasiowapa wafanyakazi mikataba, wasioheshimu haki za binadamu na kudhalilisha watumishi wao.

Wanashauri kuwa pamoja na kufuatilia masuala ya kodi ni vyema kuwa ukaguzi wa mikataba na hali ya wafanyakazi, huku wakipendekeza Maofisa Vijana wilayani kusaidia jukumu hilo eneo ambao halina maofisa kazi.

Nyoso Mapunda, ni Ofisa Vijana Wilaya ya Mafia, anasema wakati mwingine, wilaya hazina ofisakazi au yuko makao makuu , hivyo ni vyema kuwatumia maofisa vijana kufanya ukaguzi kwenye upungufu.

### DESKI RUSHWA YA NGONO

Suala la rushwa ya ngono hasa kwa wanawake wafanyakazi lilijadiliwa kwa kina ikidaiwa kukithiri na ili kupata ufumbuzi washiriki wanasema ni vyema kuwe na dawati la kuripoti taarifa za rushwa hiyo sehemu za kazi.

Washiriki hao wanataka kuwe na sera au maagizo ya kuwa na utaratibu wa kuwa na dawati linaloshughulikia rushwa ya ngono sehemu za kazi ambalo litawashirikisha vyama vya wafanyakazi, litawasaidia wanawake kufikisha kesi kwenye mamlaka zinazohusika.

### JITIHADA SERIKALI

Ofisa Miradi wa Action Aid, Levina Nawenzake, akizungumza kwenye mkutano huo, anasema wadau wanazipokea jitihada za kuandaa mpango wa kitaifa wa ajira zenye staha, ambao ulitangazwa kwenye mkutano huo wa vijana na maofisa kutoka Wizara ya Kazi.

Anawaambia washiriki kuwa kitisho cha ajira zisizo na staha ni matokeo utandawazi na ukosefu wa ajira lakini ni lazima serikali iangalie na kulinda maslahi na afya za wananchi.

Aidha, anashauri kuitizama sekta isiyo na rasmi na zote zenye ajira duni, lakini pia taasisi za umma zinazosimamia kazi na wajibu wa waajiri kuwajibika kulinda maslahi ya waajiriwa.

Jovina, anasema malalamiko ya rushwa ya ngono kukithiri ni matokeo ya baadhi viongozi kutumia mamlaka yao kuwahadaa na kuwanyanyasa wafanyakazi wanawake ambao pamoja na kutumiwa kingono, hulipwa ujira mdogo, hufanyakazi zisizo na staha zisizo na mikataba na kwamba ufumbuzi ni kuanzisha na kusimamia utekelezaji wa mpango wa taifa wa kazi zenye staha.

MAKALA

# Ujerumani inavyowakomboa walemavu Mara

**Na Sabato Kasika**

SERIKALI ya Ujerumani imeongeza nguvu katika mradi wake wa kusaidia wanafunzi wenye ulemavu kupata elimu bora wakiwa shuleni kwa kutoa fedha, vifaa mbalimbali vya kujifunzia na chakula.

Mradi huo unaofahamika kama BMZ unatekelezwa katika kata 20 za wilaya za Musoma na Rorya mkoani Mara.

Mbali na wanafunzi, Kundi lingine linalonufaika katika mradi huo ni watu wenye ulemavu walioungana katika vikundi vya ujasiriamali na miradi ya uzalishaji mali.

Meneja wa mradi huo nchini, Niwaely Sandy, amesema mpango huo unalenga katika kata hizo ili kuhakikisha jamii zenye mahitaji zinaendelea kupata huduma muhimu kama elimu na chakula.

"Kuna suala la sera jumuishi kwa wenye ulemavu katika nyanja ya elimu, hivyo hatuna budi kuwasaidia kwa hali na mali katika kujenga uwezo wao kuanzia ngazi ya elimu hado kwenye familia kuinua kipato chao," anasema Sandy.

Sandy anasema, mwaka huu mradi huo umesaidia kiasi cha Sh. milioni 16, na kunufaisha kata za Bugwema, Bukima, Bukumi, Bwasi, Kiriba, Makojo, Murangi, Nyambono, Nyamrandirira na kisiwa cha Suguti.

" BMZ ni mradi wa serikali ya nchi ya Ujerumani ambao unahusisha mambo ya uchumi inalenga kusaidia familia ziwe na uwezo wa kujihudumia katika mahitaji muhimu ya kila siku," anasema.

Anasema, Hospitali Teule ya Shirati ni ya Kanisa la Mennonite (KMT), ambalo ni mdau wa mradi huo unaowezesha watu wenye ulemavu kutoka Wilaya ya Musoma hasa vijijini na Rorya.

"Kila mwaka shule zinapofunguliwa, mradi wa BMZ umekuwa ikitoa msaada huo kwa wanafunzi wenye ulemavu, ili wapate elimu bila kukabiliwa na changamoto za uhaba wa vifaa na chakula," anasema.



Baadhi ya walemavu wa Kata ya Makojo waliopata msaada. **PICHA ZOTE: MPIGA PICHA WETU**

**MRADI KUANZA**

Sandy anasema, mradi wa BMZ ulianza nchini mwaka 2017 kwa kutambulisha kwa Mganga Mkuu wa Mkoa wa Mara, Wakurugenzi wa pamoja na Maofisa ugani kutoka wilaya zote mbili.

"Viongozi hawa walipata elimu ya mradi kutokaWizara ya Vijana, Ajira, Kazi na Watu wenye Ulemavu wakishirikiana maofisa mradi," anafafanua.

Anasema, takwimu ya sensa ya mwaka 2012 inaonyesha kuwa mkoa wa Mara ina watu wenye ulemavu 4,580, jambo ambalo wanahitaji usaidizi.

Anasema, baada ya mradi huo kufanya utafiti watu 5,444 walibainika kutoka wilaya hizo mbili.

Mradi huo umefanikiwa kuwapa vifaa mbalimbali ikiwamo baiskeli na simu za mkononi kila moja kwa ajili ya mawasiliano.



Meneja wa mradi wa BMZ, Niwaely Sandy.

Pia mradi uliwezesha upatikanaji wa madaktari ambao walitoa huduma ya uchunguzi wa kiafya kwa watu 3,512.

**UJASIRIAMALI**

Meneja huyo anasema, mwaka 2018, vikundi 20 vya ujasiriamali kila kata viliundwa na kupewa mafunzo, kisha kusajiliwa kabla ya kupewa fedha Sh. 500,000 kwa kila kikundi.

"Toka tuanze kuviinua vikundi vya ujasiriamali hadi sasa vinaendelea vizuri," anaingeza.

**HUDUMA YA AFYA**

Anafafanua kuwa mwaka jana, watu 200 wenye ulemavu kati ya wale waliofanyiwa upimaji walipelekwa Hospitali ya Shirati na kufanyiwa upasuaji wa mifupa ili kurekebisha viungo.

Urekebishaji huo uliwahusu hasa watoto, ilifanywa kwa ushirikiano na daktari bingwa wa mifupa wa Hospitali ya Bugando Mwanza.

"Awamu hii ya kwanza ya upimaji watu 200 wa kufanyiwa upasuaji wa marekebisho, lakini kuna mahitaji makubwa tatizo ni ufinyu wa bajeti," anasema.

Mbali na hilo, anasema, wametengeneza miguu bandia 20 kwa ajili ya watu wenye ulemavu, katika wilaya hizo mbili na pia miwani kwa walengwa 30.

"Mradi pia umefungua ofisi za SHIVYAWATA wilaya na kuwanunulia vifaa vya ofisi kama kompyuta, mashine za kudurufu na samani. Pia tunatoa pesa za kuendeshea ofisi kila mwezi pamoja na kulipa kodi ya pango na tumetafuta wadau wa kuwasaidia watoto wenye vichwa vikubwa na mgongo wazi 17 kupata huduma zao," anasema.

Anasema, kutokana na idadi ya watu wenye ulemavu kuwa kubwa kuliko hata ile ya sensa ya 2012, wanaiomba serikali iwasaidie kwa uhitaji vifaa vya kujimudu kama vile baiskeli, miguu bandia, miwani, fimbo nyeupe, vifaa vya kusaidia kusikia na miwani.

# MGUNDUZI WA CORONA AFARIKI

## ■Ujumbe wake wa tahadhari ulionekana uongo
## ■Mkanganyiko wa kifo waleta hasira

**Na mwandishi wetu**

DAKTARI raia wa China ambaye alijaribu kutoa tahadhari kuhusu mlipuko wa virusi vya corona amefariki Dunia katika hospitali akipatiwa matibabu.


Mtaalamu huyo wa tiba za binadamu, Li Wenliang amepata maambukizi wakati akifanya kazi katika hospitali mjini Wuhan, jimbo ambalo chanzo cha ugonjwa huo.

Kabla ya kusambaa kwa virusi hivyo, Wenling alituma ujumbe wa tahadhari kwa madaktari wenzake Desemba 30 mwaka huu, lakini alizuiwa.

Katika kumkatisha tamaa, mamlaka ya polisi ilimuamuru kuacha kutoa taarifa na maoni yake walioita ya uongo.

Hata hivyo, taarifa ya kifo chake imekuwa ya kukanganya, lakini inadaiwa na vyombo vya habari kuwa alifariki usiku wa kuamkia Ijumaa.

Virusi vimeua watu 636 na watu 31,161 wameambukizwa nchini China. Hiyo ni kwa mujibu wa tume ya taifa ya afya.Vifo hivyo vinahusisha 73 ambavyo vimeripotiwa siku ya Alhamisi.



**LI WENLIANG NANI?**

Dokta Li, aliweka habari kwenye mtandao wa Weibo akiwa kitandani hospitalini mwezi mmoja baada ya kutuma ujumbe wa tahadhari.

Daktari huyo mwenye miaka 34 aligundua visa saba vya maambukizi ya virusi ambavyo alifikiri kuwa vilifanana na Sars, mlipuko uliowahi kutokea mwaka 2003.

Desemba 30 alituma ujumbe kwa madaktari wenzake akiwatahadharisha kuvaa vifaa vya kujikinga kuepuka maambukizi.

Siku nne baadae aliitwa na idara ya usalama ambapo aliamriwa kusaini barua. Katika barua hiyo alikuwa akishutumiwa kutoa taarifa za uongo ambazo zimeleta taharuki miongoni mwa jamii.

Alikuwa mmoja kati ya watu nane ambao polisi walisema walikuwa wakichunguzwa kwa makosa ya kueneza uzushi, lakini baadae walimuomba radhi Dokta Li.

Katika taarifa aliyoiweka kwenye mtandao wa Weibo alieleza namna alivyoanza kukohoa mwezi Januari, siku iliyofuata alipata homa na siku mbili baadae alikuwa hospitalini. Aligundulika na virusi vya Corona Januari 30 mwaka huu.

**CHINA WAMEPOKEAJE?**

Ghadhabu na huzuni zilitanda kwenye mtandao wa kijamii wa pale taarifa za kifo cha Dokta Li zilipotangazwa siku ya Alhamisi.

Hashtag zikisema "Serikali ya Wuhan inapaswa kumuomba radhi Dokta Li" na "tunataka uhuru wa kujieleza".

Ujumbe wote huo ulianza kufuatiliwa na BBC ilipoanza kufuatilia mtandao wa Weibo siku ya Ijumaa asubuhi ikakuta ujumbe wa kampeni hizo na maoni yakiwa yameondolewa.

Sasa wengi wamekuwa wakiandika ujumbe wa kukosoa serikali bila kumtaja dokta Li moja kwa moja, lakini yote haya yanadhihirisha hasira ya raia wa China dhidi ya serikali.

"Usisahau jinsi unavyojisikia hivi sasa. Usisahau hasira hii. Hatupaswi kuacha hili litokee tena," mtu mmoja alieleza kwenye mtandao wa Weibo.

"Ukweli siku zote utaelezwa kuwa habari ya uzushi. Mpaka lini mtadanganya? Bado mnadanganya? kitu gani kingine mnachopaswa kuficha?" mwingine alisema.

**MKANGANYIKO WA KIFO**

Gazeti la kila siku la Global times na vyombo vya habari vingine nchini China viliripoti kifo cha Dokta Li siku ya Alhamisi.

Global Times liliandika katika ukurasa wake wa twitter ukisema kuwa kifo cha Dokta Li kimeleta majonzi nchini China.

Waandishi wa habari na madaktari ambao hawakutaka kutajwa majina yao waliambia BBC kuwa maofisa wa serikali waliingilia kati.

Vyombo vya habari rasmi viliambiwa vibadilishe ripoti zao ziseme kuwa daktari bado anapata matibabu.

Vyombo vya habari baadae viliripoti muda mwingine wa kifo cha Dokta Li.

**HALI IKOJE?**

Ingawa virusi vimesambaa mpaka nje ya China, kukiwa na ripoti ya maambukizi kwenye mataifa 25, mpaka sasa kumeripotiwa vifo viwili nje ya China, ikiwa mtu mmoja Hong Kong na mtu mmoja Ufilipino.

Shirika la afya duniani, WHO limetangaza mlipuko wa virusi vya Corona kuwa janga la kiafya, likisema ikiwa fedha hazitaelekezwa kupambana na mlipuko, mataifa yatajutia hilo baadae.

Ingawa takwimu rasmi nchini zinasema kuna maambukizi yamefikia watu 31,000, baadhi ya wanasayansi wamekisia kuwa idadi inaweza kuwa mara 10 zaidi, kwa kuwa wengi wao huonyesha dalili polepole, na hawapati matibabu, na hivyo kuwaambukiza wengine.



HABARI KIMATAIFA

# Marekani yajigamba kuua kiongozi wa Al-Qaeda

**WASHINGTON, Marekani**

KIONGOZI wa Marekani, Donald Trump, ametangaza kikosi chake kimemuua kiongozi wa kikundi cha Al-Qaeda katika eneo la Rasi ya Uarabuni.

Qasim al-Raymi aliyeongoza kikundi cha Jihad tangu mwaka 2015, aliuawa wakati wa operesheni ya majeshi ya Marekani nchini Yemen, Ikulu ya Marekani imeeleza.

Kiongozi wa wapiganaji wa Jihad amekuwa akihusishwa na mfululizo wa mashambulizi dhidi ya maslahi ya nchi za Magharibi katika miaka ya 2000.

Alichukua madaraka ya uongozi baada ya mtangulizi wake kuuawa kwa shambulio la ndege zisizo na rubani za Marekani.

Kundi hilo la AQAP liliundwa mwaka 2009 kutokana na matawi mawili ya Al-Qaeda nchini Yemeni na Saudi Arabia, ikiwa na nia ya kuangusha tawala za serikali zinazoungwa mkono na Marekani na kuondoa ushawishi wa nchi za Magharibi kwenye ukanda huo.

Tetesi kuhusu kifo cha al- Raymi kutokana na shambulizi hilo la Marekani zilianza kusambaa mwishoni mwa mwezi Januari.

Katika kujibu kitendo hicho, kundi hilo lilitoa ujumbe wa sauti ukiwa na sauti ya al -Raymi tarehe 2 mwezi Februari ukisema kuwa wao ndio waliotekeleza shambulio la risasi kwenye kambi ya jesho la wana maji wa Marekani huko Pensacola, Florida.

Shambulio hilo lilifanyika mwezi Desemba, na ujumbe huo huenda ulirekodiwa mapema.

Taarifa kutoka Ikulu ya Marekani sasa imethibitisha kifo cha al-Raymi lakini haijasema aliuawa lini.

"Kifo chake kinaendelea kudhoofisha kundi la AQAP na shughuli za kundi la al-Qaida, na inatufanya tuendelee kukaribia kuondosha vitisho vya makundi haya yanayohatarisha usalama wa taifa," taarifa ilisomeka.

"Marekani, maslahi yetu na washirika wetu wako salama kutokana na kifo chake".

***BBC***



Wataalam wa Wakala wa Anga ya Juu ya Marekani (NASA), wakimsaidia mwanaanga pekee mwanamke, Christina Koch, muda mfupi baada ya kutua ardhini na chombo cha Urusi cha Soyuz MS-13, kusini mwa Zhezkazgan katika mkoa Karaganda nchini Kazakhstan. **(PICHA: REUTERS)**

# Majeshi ya Syria yaingia mji muhimu

VIKOSI vya serikali ya Syria, vimeingia kwenye mji wa kimkakati wa Saraqeb ambao ulikuwa ngome ya mwisho ya waasi.

Kufanikiwa kuingia eneo hilo ni baada ya mapambano makali na wapiganaji wa upinzani.

Operesheni za vikosi vya Rais Bashar al-Assad kwenye miji na vijiji vya kaskazini magharibi mwa jimbo la Idlib zimesababisha zaidi ya watu laki tano kukosa makaazi kwa zaidi ya miezi miwili, hali inayozidisha janga la kibinaadamu kwenye ukanda huo wenye wakimbizi wa ndani.

Hatua hiyo imeikasirisha Uturuki na kuhatarisha kuzuka mapambano ya kijeshi kati ya majeshi ya Uturuki na Syria.

Mji wa Saraqeb ulioko karibu na mpaka wa Uturuki, umekuwa kitovu cha mapambano makali kwa siku kadhaa.

Wakati huo huo, wizara ya mambo ya nje ya Urusi, imesema kuwa ujumbe wa nchi hiyo kesho utaelekea Uturuki kwa ajili ya kuijadili hali katika jimbo la Idlib

***DW***

## Trump kusherehekea ushindi Ikulu

**WASHINGTON, Marekani**

RAIS wa Marekani, Donald Trump, amefurahia ushindi baada ya kuondolewa mashtaka na Bunge la Seneti katika mashtaka mawili yaliyokuwa yakimkabili.

Kiongozi huyo alifanya hafla ndani ya Ikulu ya Marekani na kuwaponda wapinzani wake wa kisiasa.

"Nimefanya makosa kwenye maisha yangu, nitakiri.. lakini haya ndio matokeo, " alisema huku akinyanyua gazeti lililokuwa na kichwa cha habari "Trump hana hatia".

"Tumepita kubaya, hatukutendewa haki.Hatukufanya kosa lolote, ulikuwa uovu, ilikuwa rushwa." Alisema akiwa Ikulu

" Sasa tuna neno zuri. Sikufikiria kama litakuwa zuri namna hii, linaitwa kusafishwa kabisa." aliongeza

Trump alishtakiwa na bunge la wawakilishi mwezi Desemba kwa matumizi mabaya ya madaraka na kulizuia Bunge kutekeleza majukumu yake, lakini hakukutwa na hatia siku ya Jumatano baada ya mchakato wa majuma mawili wa kesi dhidi yake kwenye bunge la seneti.

Kiongozi huyo pia alieleza kuhusu uchunguzi uliokuwa ukifanyika kuhusu kampeni za uchaguzi wa mwaka 2016 na uhusiano na Kremlin.

"Ulikuwa upumbavu mtupu, hili suala halipaswi kutokea tena kwa rais atakayefuata." Alisisitiza.

Trump alisema kuwa bado ana imani na chama cha Republican wakati huu wakielekea kwenye uchaguzi ujao wa mwezi Novemba.

Hata hivyo, kufanyika kwa sherehe baada ya kusafishwa kwake, kulitofautiana na rais Bill Clinton ambaye alihutubia mwaka 1999, alipoomba radhi kwa raia wa Marekani, baada ya kushtakiwa.

"Ninataka kusema tena kwa raia wa Marekani ninaomba radhi kwa kile nilichokisema na kwa mzigo mkubwa walioubeba wabunge na raia wa Marekani kwa ujumla," Bwana Clinton alieleza.

**BBC**

# Wanafunzi 6 walifariki kwa kukosa hewa

**NAIROBI, Kenya**

MATOKEO ya upasuaji yanaonesha kwamba wanafunzi sita kati ya 14, waliofariki katika mkanyagano siku ya Jumatatu jioni Magharibi mwa Kenya, walikosa hewa.

Daktari anayehusika na uchunguzi wa maiti, Dickson Mchana, alisema kundi lake la maofisa bado linaendelea na uchunguzi kuhusu sababu za vifo vya wanafunzi wengine wanane ambao pia walifariki katika mkanyagano huo katika shule ya msingi ya Kakamega.

"Tunaharakisha uchunguzi ili kutoa matokeo kwa lengo la kuandaa miili ili ichukuliwe na familia kwa ajili ya ibada ya mazishi itakayofanyika katika uwanja wa Bukhungu mjini Kakamega", alisema Dkt Mchana.

Maofisa wa polisi bado wanachunguza kisa hicho ambapo wanafunzi 14 walifariki huku wengine 39 wakijeruhiwa.

Wamerekodi taarifa kutoka kwa walimu , wanafunzi na mashahidi ili kubaini kilichosababisha mkasa huo.

Wanafunzi wawili wanaendelea kupata matibabu katika hospitali kuu ya Kakamega.

Waziri wa elimu George Magoha, alifunga shule hiyo hadi siku ya Jumanne wiki ijayo.

Mkanyagano huo ulitokea katika shule ya upili ya Kakamega , Kaskasini Magharibi mwa Nairobi wakati wanafunzi hao wapolikuwa wakitoka shuleni

Mkuu wa kituo cha polisi cha Kakamega, David Kabena, alisema kuwa wanafunzi wengine 39 walijeruhiwa wakati wa mkasa huo.

Imedaiwa kwamba baadhi yao walianguka kutoka ghorofa ya tatu ya jengo hilo walipokuwa wakitoka darasani.

Ripoti ambazo hazijathibitishwa zinasema kuwa wanafunzi wawili walipelekwa katika chumba cha dharura katika hospitali iliyopo kaunti ya Kakamega.

Wazazi walikusanyika hospitalini na shuleni hapo wakiwa na hofu kuwa inawezekana kuna wanafunzi wengi zaidi wamejeruhiwa.

***BBC***

# HADITHI

# Jumba Jekundu-39

WASWAHILI wana msemo wao unaosema kuwa ufukara ni jereha la ulimwengu. Wakiwa na maana, mtu fukara mara nyingi hukutana na mitihani mikubwa duniani, ambayo mingi husababishwa na baadhi ya binadamu wengine wenye vipato kwa kuwaona hawana thamani na hawahitajiki kuwa na kitu chochote cha thamani.

Kijana anayetoka kwenye familia duni Kadili, anatokea kupendwa na msichana mrembo anayetoka kwenye familia ya kitajiri, Edina.

Lakini kitendo hicho kinamsababishia kijana huyo matatizo makubwa ambayo hajawahi kuyapata katika maisha yake, kiasi cha maisha yake kuwa hatarini. Fuatilia mkasa huu wa aina yake.

**Na Adam Fungamwango, (0716 350534)**




"Nadhani umenisikia, lakini bado hujanijibu Meze." Kadili alimshtua rafiki yake.

"Ni kweli Kadili, mimi sina mpenzi, umri wa kuona tayari, lakini haya ni mambo ya kujipanga."

"Kama muoaji yupo na muolewaji yupo, mengine niachie mimi, ninachotaka ukubali, ila kama umempenda."

"Hakuna mwanaume yoyote anayeweza kumkataa Eliza, ila yeye atakubali kweli na wazazi wake, hasa mama yako atakubali?"

"Hilo pia niachie mimi."

"Basi akikubali mimi sina tatizo." Meze alithibitisha kuwa anaweza kumuoa Eliza."

Marafiki hao waligongeana mikono. Ghafla moyo ya Meze ulifarijika, kwani alikuwa anampenda Eliza kutokana na urembo, umbile na hata tabia yake ya upole, lakini alikuwa akifungwa na kuwa alitakiwa kuwa mke wa rafiki yake Kadili baadaye, lakini mambo yamebadilika.

**********************************

Ilikuwa ni saa sita mchana. Ni muda ambao jiji la Dar es Salaam kwa sehemu kubwa ya majira yake huwa ni joto la 'kufa mtu'. Sebuleni alikuwa amekaa Kadili. Pembeni yake alikaa dada yake binamu Eliza. Ni msichana ambaye awali alipwaswa awe mke wake kama ingeshindikana kabisa kumpata Edina.

Nyumba yao haikuwa na umeme, hivyo jua kali lilikipiga bati la nyumba hiyo lililopo juu na kutengeneza joto kubwa lililowafanya kijasho kiwamiminike.

"Nimekwita hapa nina ujumbe wako muhimu Eliza." Kadili alianza kumueleza aliyemwita.

"Ujumbe gani kaka."

"Ni ujumbe kutoka kwa Meze."

Eliza alishtuka. Hakutegemea kitu kama kile. Hakutegemea ujumbe wowote wa Meze, basi autume kupitia Kadili.

Anakumbuka kukutana mara kwa mara na Meze na kutaniana kama mashemeji, lakini si zaidi ya hayo.

"Eliza kama unavyokumbuka kuwa wewe ulikuja hapa kwa kazi maalum ambayo haikufanikiwa.

Ni kwamba mama na baba yako walikuleta hapa kwa ajili yangu baada ya kuona nasumbuliwa sana na familia ya kina Edina, hasa wakati huo mama yake yu hai.

Kwa sasa amefariki kwa bahati mbaya na kama unavyoona tayari shemeji yako mtarajiwa alikuja hapa na ametualika Jumamosi." Alisema na kumtazama kwa makini Eliza ambaye mpaka wakati huo bado uso wake ulionyesha mshangao.

"Kazi kubwa umeifanya hapa kwa kunitunza, kumtunza mama wakati unasubiri na pia umepoteza muda mrefu sana hapa, sasa binafsi nimeona kuwa si busara ukaondoka tu hivi hivi."

"Ndiyo kaka, unataka unipe nini niondoke nacho kwetu Mtoni Mtongaji?" Aliuliza Eliza kimzaha huku ile kiu ya kutaka kujua kitu ikiwa bado kwenye usao wake.

"Kwani nikuulize, huko ulikotoka ulikuwa na mpenzi au mchumba?"

Eliza alingua kicheko cha aibu, akaondoa sura yake kwa Kadili na kujibu.

"Ningekuwa na mpenzi au mchumba nisingekuja huku. Kumbuka kaka nilikuja kwa sababu yako ili niolewe na wewe kama kaka yangu binamu, na nilikubali, kama ningekuwa naye, sidhani kama ingekuwa hivyo."

"Sitaki uondoke bure nataka nikupe mume, uko tayari au unataka utafute mwenyewe?"

"Mhh mimi hapa hata sijui niseme nini. Niko njia panda kaka. Hakuna mwanamke ambaye hataki kuolewa, ila tatizo ni kwamba naolewa na nani."

"Kwani ulikuwa unataka mwanaume wa aina gani?" Kadili aliendelea kumtega.

"Ilikuwa kama wewe hivi, lakini ndiyo imeshindikana."

"Nikikuletea mwanaume kama mimi, utamkubali?"

"Kama wewe kivipi?"

"Kitabia, mwenendo na vitu vinginevyofanana na mimi."

"Wa aina hiyo siwezi kumpinga, nitamkubali."

"Basi yupo."

"Nani?"

"Meze."

Aliposikia jina hilo, Eliza alibaki kimya kwa sekunde kadhaa.

Meze ni shemeji yake. Ni mwanaume ambaye mara kwa mara wakikutana hutaniana.

Akakumbuka moja ya mambo ambayo walizungumza na kuleta mtafaruku kwa shangazi yake mama Kadili.

Akakumbuka siku hiyo alipokwenda dukani kwa Meze kumuulizia Kadili.

"Kadili hata mimi sijamuona muda mrefu sasa." Alijibu Meze na kuongeza.

"Mimi nilidhani uko naye nyumbani huko."

"Hapana aliondoka muda mrefu sana, mpaka saa hizi inafika saa tatu usiku bado hajaonekana."

"Eliza wacha wivu, mumeo mtarajiwa atarudi tu, au unadhani yuko na wanawake wengine?' Alihoji.

"Mhh, hapana usalama wake muhimu kwanza."

"Siyo wivu bibie?"

"Hapana sina wivu kwa sababu sidhani kama rafiki yako ananipenda hasa."

"Kwa nini?"

"Huo unafiki, hata wewe unajua hilo. Kuna mtu anampenda, ndiyo anayemsumbua, na mimi nimekuwa kama mbadala tu, ikishindikana kabisa ndiyo anioe mimi."

"Sasa hilo linakukwaza?"

"Sana tu, nimekubali kwa sababu wanaotaka hili litimie ni shangazi yangu, mama yake Kadili na baba yangu mzazi mzee Tengeneza, kaka yake shangazi, vinginenvyo nisingekubali."

"Ila kuolewa unataka?"

"Meze, hakuna mwanamke asiyekubali kuolewa. Lakini anataka kuolewa na mwanaume anayempenda na kumjali, lakini kwangu mimi kwa Kadili ni kama spea tairi ambalo linasubiri lingine liharibike, ndiyo litumike, kama halikuharibika ndiyo basi tena."

"Kama mimi nigekuwa Kadili, saa hizi ningekuwa nimeshakuoa." Maneno hayo yalimtoka Meze bila kutarajia.

"Inawezekana wewe unajua thamani yangu na si rafiki yako."

"Hakika, Eliza wewe ni mwanamke mrembo, mwenye kila sifa ya kuwa malkia ndani ya nyumba. Bahati hii haikunikuta mimi, nisingeipoteza."

"Haijakukuta kwa sasa, lakini huenda baadaye ikakukuta." Alijibu Eliza.

"Nikipata mume kama yule si nitaringa." Alijisemea mwenyewe.

"Mbona hunijibu Eliza?" Sauti ya Kadili ilimshtua kutoka kwenye lindi la mawazo akiikumbuka siku hiyo na kuchambua neno moja baada ya jingine.

Ni kweli baada ya siku ile Eliza alionekana kama kuvutiwa na Meze. Lakini tena siku ambayo walimsindikiza Edina na alipokuwa anaaga alikumbatiana na Kadili, macho yake yalikumbana ana kwa ana na Meze. Hayakuwa macho ya kawaida. Yalionyesha mapenzi ndani yake. Tena mapenzi ya dhati. Eliza na yeye ndani ya moyo wake alitaka akumbatiwe. Lakini haikuwezekana. Lakini Kadili alionekana kama kuhisi kitu ndani ya moyo wa kile mmoja.

"Kwani mwenyewe anasemaje? Umeshamwambia?" Lilikuwa ni jibu la Eliza.

Aliuliza swali badala ya kujibu kwa sababu yeye ni mtoto wa kike. Haiwezekani akakubali, halafu baadaye mwanaume akakataa, itakuwa ni aibu kubwa.

"Nimeshaongeza na Meze. Amekubali na yuko tayari kutoa barua ya uchumba na hatimaye kukuoa kabisa." Kadili alimtoa hofu.

"Shangazi je najua hili?" Eliza bado alionekana kuwa na wasiwasi.

"Kumbuka mama yeye alikuwa anataka wewe uwe mke wangu, lakini imeshindikana, sidhani kama atakataa wewe tena kuolewa na mtu mwingine, tena umemchagua mwenyewe, anayemfahamu, lakini pia ni rafiki yangu mkubwa. Ina maana hujaenda mbali."

"Sawa kaka hapo nimekubali."

Kadili alinyanyuka na kumnyayua Eliza akamkubatia kwa nguvu.

"Asante mchumba wangu wa zamani kwa kukubali kuolewa."

Eliza alijikuta akiangua kicheko cha nguvu kwa maneno hayo.

"Eee bwana, mzigo siyo wangu tena, ni wa Meze."

"Ndiyo na mimi haukuwa wangu tena ila ni wa Edina." Eliza alijibu na kuendeleza vicheko.

Ghafla mama Kadili aliingia na kukuta wako kwenye hali hiyo. Ilimshangaza na kumshtusha.

Vijana wake wawili, mmoja kijana wake na mwingine mtoto wa kaka yake ambao alitaka waoane, lakini haikuwezekana kutokana na mazingira jinsi yalivyokuwa.

Cha ajabu leo anawakuta wamekumbatiana laivu, tena kwa vicheko na bashasha. Hakujua nini kimetokea.

"Wamependana ghafla?" Alijiuliza. Kiasi ilimfariji kwa sababu alitaka iwe hivyo.

Aligeuka na kurudi alikotoka kwa sababu hakutaka kuwavuruga watoto wake. Kadili na Eliza walimuona, lakini kabla ya kufanya chochote walimuona akirejea anakotoka na macho yake yakijifanya kama hajaona kitu.

Wakatazamana na kuangua tena kicheko cha nguvu zaidi kuliko cha mwanzo na mama akashtukia kuwa walimuona.

***Itaendelea Jumamosi***

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## MATANGAZO MCHANGANYIKO

**ANAHITAJIKA MUUGUZI**
Anahitajika muuguzi msaidizi au Nurse Assistant kwa anayehitaji
**Apige: SImu Namba:**
**0786 641903 au 0716 172929**

**MKOPO WA HARAKA NA KUTOKA ENTERPRISE FINANCE LIMITED (EFL)** Kwa mahitaji kama kulipa ada ya shule, kodi, kuboresha biashara, kumaliza tenda etc. Kwa maelezo zaidi piga: **0758 112 332. Karibu EFL**

**NIPASHE NI JIBU LAKO**
**NJOO UTANGAZE NASI**
**BIDHAA YAKO**
**KWA BEI NAFUU SANA**

## PASSPORT IMEPOTEA



**ZUBERI DAUDI LOLO** anatangaza kupotelewa na Hati ya Kusafiria (Passport) yenye namba **AB 458872.** iliyotolewa na Idara ya Uhamiaji Makao Makuu Dar es salaam mwaka 2011. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilicho karibu. Taarifa ya polisi: **KAWE/RB/364/2020.**

115621502

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**DENIS LUCAS KILUMBA**
Anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T334DCL**
Chassis No
**JCG150003234**
Engine No **1JZJAA13234**
Kwa taarifa ya polisi
**ARU/ARU/RB/122489/2020**
Au piga simu namba
**0658051512**

215621802

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**PERPETUA JOHN BILINZOZI** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 894 DEE TOYOTA RAUM.**
Chassis namba
**NCZ200095394.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.
Taarifa ya polisi:
**DAR/GOG/RB/523646/2019.**

115621402

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF DODOMA AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. .........OF 2020**

**In the matter of the Estate of the Late JOVINE ALOYCE MFOY of Kisasa, within Dodoma Municipality**

**And**

**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTER OF ADMINISTRATION BY HAPINESS EMANUEL MAINA**

**GENERAL CITATION**
**(RULE 75 PROBATE RULES GN 369 OF 1963)**

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the estate of the above named deceased person are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letter of Administration is made to the above named petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 10 Day of February, 2020.

**Dated at Dodoma this 05 Day of February, 2020.**

RESIDENT MAGISTRATE
RESIDENT MAGISTRATE DODOMA DISTRICT

215621101

**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676**

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676

Nipashe
MWANGA WA JAMII
www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.



# STERLING AIPA PIGO CITY

**MANCHESTER, England**

RAHEEM Sterling ataukosa mchezo wa Manchester City dhidi ya West Ham utakaochezwa kesho baada ya kuthibitishwa kwamba mshambuliaji huyo wa England ameumia misuli.

Pigo hilo la Sterling lilikuja wakati City walipofungwa na Tottenham wikendi iliyopita, na haijatolewa taarifa zaidi kwa muda gani atakuwa nje ya dimba.

Imebakia kuwa jambo la kusubiriwa kuona kama Sterling atapona haraka na kuiwahi mechi dhidi ya Leicester itakayopigwa Februari 22, mwaka huu au mchezo wa hatua ya 16 bora wa Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Real Madrid siku nne baadaye.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na tovuti ya City: "Raheem Sterling ataukosa mchezo dhidi ya West Ham baada ya vipimo kuonyesha kwamba aliumia misuli ya mguu wa kushoto.

"Raheem aliumia kwenye mchezo dhidi ya Tottenham Jumapili wakati zikiwa zimesalia dakika sita na alifanyiwa uchunguzi Alhamisi kwenye akademi ya City.

"Ataendelea kupatiwa matibabu kipindi cha mapumziko ya baridi. Kila mmoja ndani ya City anamtakia heri Raheem apone haraka."

City itaanza likizo ya muda mfupi baada ya mchezo wake dhidi ya West Ham, huku kikosi hicho cha kocha, Pep Guardiola ambacho kipo nafasi ya pili nyuma ya Liverpool, kitarudi dimbani siku 13 baadaye kucheza dhidi ya Leicester.

Sterling amefunga mabao 11 katika mechi 23 za Ligi Kuu kwa City msimu huu.

## LUIZ: ARTETA AMERUDISHA MASHABIKI ARSENAL

**LONDON, England**

DAVID Luiz amemsifia kocha mpya wa Arsenal, Mikel Arteta kwa kuwarudisha "mashabiki" kwenye klabu, akibainisha kikosi kilikuwa na "huzuni" chini ya mtangulizi wake, Unai Emery.

Arteta alichukua nafasi ya Emery Desemba mwaka jana akitoka kuwa msaidizi wa Pep Guardiola pale Manchester City na klabu ilionekana kutokuwa kwenye kiwango chake.

Ingawa Arsenal imeshinda mechi tatu tu kati ya tisa chini ya Arteta katika mashindano yote, lakini Luiz anaona kuna mabadiliko yaliyowafanya wachezaji kuimarika zaidi.

"Kwa uhakika kabisa mambo yamebadilika na morari ya wachezaji ipo juu zaidi hapa Arsenal kwa sasa," alisema raia huyo wa Brazil akinukuliwa na tovuti ya klabu hiyo.

"Kama unalala saa nne kwa furaha, utalala vizuri zaidi ya saa nane. Hivyo Arteta ameweza angalau kurudisha ari ya mashabiki uwanjani."

## United yamweka Pogba sokoni

**MANCHESTER, England**

MABOSI wa Manchester United wameshusha kiasi cha pauni milioni 30 kutoka katika thamani ya awali ya Paul Pogba na sasa inamaanisha ' taa ya kijani imewaka' ya kiungo huyo wa Timu ya Taifa ya Ufaransa kuondoka klabuni hapo katika dirisha la majira ya joto litakapofunguliwa.

United ilizuia kila njia kwa mahasimu wake waliokuwa wanataka kumsajili mshindi huyo ya Kombe la Dunia katika majira ya joto mwaka jana, huku Ole Gunnar Solskjaer alipokuwa anapambana kukijenga kikosi chake kwenye safu ya kiungo.

Sasa baada ya kutua kwa Bruno Fernandes, uwezekano wa Pogba ambaye kwa sasa ni majeruhi upo, na United iko tayari kukaa mezani kufanya biashara na timu yoyote inayomhitaji, limeandika gazeti la Sun.

Imeripotiwa kuwa mabosi wa United ambao walikuwa wanapambana kuhakikisha wanambakisha Pogba, sasa wamekubali kumruhusu kiungo huyo kuondoka baada ya kubaini uamuzi huo hautaiathiri klabu hiyo ya Old Trafford.

Hata hivyo United bado inataka kupata faida kubwa kwa kumuuza mchezaji huyo ambaye Agosti mwaka 2016 walimnunua kwa dau ghali lililoweka rekodi duniani.

United ililipa kiasi cha pauni milioni 100 kwa vigogo wa Italia, Juventus ili kunasa saini ya Pogba na ikikubali kumlipa mshahara wa pauni 290,000 kwa wiki, katika mkataba wa miaka mitano aliyosaini kuitumikia klabu hiyo.

Baada ya kufanya vizuri katika fainali za Kombe la Dunia huko Urusi, United ilitangaza thamani mpya ya Pogba ni pauni milioni 180, lakini baada ya kuweka punguzo, nyota huyo sasa atauzwa kwa dau la pauni milioni 150, ambalo bado ni faida kwa klabu hiyo.

Mfaransa huyo mwenye umri wa miaka 26 ameichezea United mechi nane tu msimu huu, kutokana na kupata majeruhi ya enka mara kwa mara.

## HABARI MICHEZO




# VINICIUS JR AKATAA KWENDA PSG

**MADRID, Hispania**

MSHAMBULIAJI wa Real Madrid, Vinicius Junior amekanusha uvumi juu ya kuhusishwa kwake na uhamisho wa kujiunga na Paris Saint-Germain, akisisitiza yeye anataka kubakia hapo Santiago Bernabeu.

Vinicius alikuwa akihusishwa kwenda PSG wakati wa dirisha dogo la Januari - huku Mkurugenzi wa mabingwa hao wa Ligi Kuu Ufaransa, Leonardo akiripotiwa kuvutiwa zaidi na Mbrazil mwenzake huyo.

Hata hivyo, Vinicius hana mpango ya kuondoka kwa miamba hao wa LaLiga, Madrid, ambako aliwasili akiwa na umri wa miaka 19 mwaka 2018.

Akizungumza baada ya timu yake kutolewa kwenye robo fainali ya Copa del Rey kwa kuchapwa mabao 4-3 na Real Sociedad, Vinicius aliwaambia waandishi wa habari: "Hakuna chaguo, nataka kubaki Madrid."

Walianza kuwa nyuma kwa 1-0 kipindi cha kwanza, baadaye Madrid wakajikuta wakifungwa 3-0 ndani ya dakika chake kipindi cha pili.

Marcelo alipunguza pengo la mabao kwa kufunga la kwanza kwa Madrid dakika ya 59, lakini Mikel Merino aliongeza la nne dakika 10 baadaye.

Licha ya mabao mawili ya Rodrygo Goes na Nacho kuifungia Madrid, lakini hayakutosha kuwafanya waibuke na ushindi kwenye mchezo huo uliopigwa katika Uwanja wa Santiago Bernabeu.

## KOCHA BARCA ATOA NENO KUTOLEWA COPA DEL REY

**BARCELONA, Hispania**

KOCHA wa Barcelona, Quique Setien anaamini klabu yake imechukua hatua zaidi, licha ya kutolewa katika mashindano ya Kombe la Copa del Rey hatua ya robo fainali Alhamisi.

Bao la Inaki Williams la dakika ya 93 liliwazima Barca na kukubali kichapo cha 1-0 kutoka kwa Athletic Bilbao katika mchezo huo.

Barca imepoteza mfululizo mechi za ugenini chini ya kocha, Setien, ambaye alichukua nafasi ya Ernesto Valverde mwezi uliopita, hata hivyo, kocha huyo amesema bado wana nafasi kwenye mbio za ubingwa wa Ligi Kuu Hispania, LaLiga.

"Tukichukulia kwa kile kilichotokea kwenye mechi zetu nje ya nyumbani, tumechukua hatua zaidi kwa kutakiwa kuimarika," alisema Setien akiwaambia waandishi wa habari.

"Ni sawa, kuna siku unakuwa na nafasi moja na unaitumia vizuri, na kuna siku unakuwa na nafasi kumi na huwezi kuzitumia. Hakuna maelezo ya kutosheleza kuelezea hili.

"Sijajua nini cha kulaumu. Goli lao lilikuja kwenye mpira ambao haukuwa na hatari. Kuna vitu ambavyo vinakuwa nje ya uwezo wako na hilo ni moja wapo.

"Kila kitu kilikwenda vizuri, isipokuwa kwa matokeo. Ninafuraha na kujituma kwa timu."

Setien aliongeza: "Tulitawala kipindi cha pili. Marc-Andre (ter Stegen) hakuokoa hatari yoyote na ilikuwa aibu kwa sababu mchezo ulikuwa chini ya utawala wetu."

## Zidane: Sijutii Madrid kutolewa

**MADRID, Hispania**

ZINEDINE Zidane anahisi kwamba kikosi cha wachezaji 11 cha Real Madrid kilichotolewa Alhamisi kwenye robo fainali ya Kombe la Copa del Rey kwa kufungwa mabao 4-3 na Real Sociedad pale Santiago Bernabeu, kilikuwa kizuri na kilitakiwa kusonga mbele.

Nyota wa Madrid, Martin Odegaard anacheza kwa mkopo Sociedad alianza kwa kufunga na Alexander Isak akafunga mawili na kuiweka mbele Sociedad kwa mabao 3-0.

Marcelo alifunga la kwanza kwa Madrid baada ya Mikel Merino kufanya matokeo kuwa 4-1, lakini Rodrygo Goes na Nacho waliotokea benchi waliongeza mawili kwa Madrid, lakini hayakutosha kuwabakiza kwenye mashindano hayo.

Hata hivyo, Zidane anaona kwamba timu iliyokuwa inaongozwa na nahodha, Sergio Ramos, na wachezaji wengine Toni Kroos, Vinicius Jr na Karim Benzema ilikuwa inatosha kuweza kusonga mbele.

"Niliweka timu ambayo nilifikiri inaweza kufanya vizuri," alisema Zidane akiwaambia waandishi wa habari baada ya mchezo huo.

"Sidhani kama tulikuwa na timu mbaya, lakini wapinzani wetu walicheza vizuri na hilo lilitugharimu sisi.

"Hapa tunakuwa pamoja, wakati tunaposhinda na pale tunapopoteza."



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# RONALDO AFUNGUKA ANGEKUWA MVUVI

**Nahodha huyo wa Timu ya Taifa ya Ureno asema bado anaamini atabeba mataji zaidi akiwa na Juventus...**

**TURIN, Italia**

CRISTIANO Ronaldo anafikiri kwamba katika umri wake wa miaka 35 angekuwa "Mvuvi wa samaki katika kisiwa cha Madeira" na anaamini anaweza kutwaa ubingwa wa Ligi ya Mabingwa Ulaya akiwa na Juventus.

Nyota huyo wa kimataifa wa Ureno alisherekea siku yake ya kuzaliwa Jumatano na aliangalia nyuma namna gani alivyoweza kuwa mmoja wa wachezaji bora wa wakati wote.

Ronaldo ameshinda taji la Ligi Kuu England, Hispania na Italia, Ligi ya Mabingwa Ulaya akiwa na Manchester United na Real Madrid, akitwaa pia taji la Mataifa ya Ulaya na lile la Ligi ya Uefa na nchi yake pamoja na kushinda mara tano tuzo ya Ballon d'Or winner.

Mafanikio hayo hayakuwa matarajio ya Ronaldo wakati alipokuwa anaota kuwa mchezaji soka.

"Katika umri wa miaka 35? Nafikiri pengine ningekuwa mvuvi kule Madeira," alisema akiiambia Canal 11.

"Hilo sikuwahi kulifikiria. Nilitaka kuwa mchezaji wa kulipwa, lakini sikudhani kama ningeshinda kila kitu nilichokishinda."

Ronaldo kwa mara ya kwanza alitwaa taji la Ligi ya Mabingwa akiwa na mashetani wekundu msimu wa 2007-08 na akashinda manne katika misimu mitano pale Madrid kati ya msimu wa 2013-14 na 2017-18.

Msimu wake wa kwanza na Juve ulimalizika kwa kushinda taji la Ligi Kuu Italia, Serie A, lakini akatolewa kwenye hatua ya robo fainali ya michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya na Ajax, ingawa bado ana matumaini ya kulibeba tena taji hilo.

"Kucheza hapa Juventus kunanipa mimi nafasi ya kushinda tena," aliongeza.

"Tunajua kwamba ni ngumu, inategemea na mambo mengi, lakini inawezekana kwa sababu tuna timu nzuri.

"Tunatakiwa kuchukua hatua moja mbele."

## KWA UFUPI

**THAMANI YA POGBA YAPUNGUA**

MANCHESTER United imepunguza kiasi cha pauni milioni 30 katika bei ya kumuuza kiungo wake Mfaransa, Paul Pogba (26), ambaye sasa atakuwa huru kuondoka klabuni hapo kwa dau la pauni milioni 150. ***(Sun)***

**ARTETA KUISUKA ARSENAL**

KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta, anajipanga kukijenga upya kikosi chake huku straika wa Timu ya Taifa ya Gabon, Pierre-Emerick Aubameyang (30), Mfaransa Alexandre Lacazette (28) na Kiungo Mjerumani Mesut Ozil (31), wanatarajiwa kuuzwa. (Sun)

**TRAORE AKARIBIA BARCA**

BARCELONA inajiandaa kufanya mchakato wa kumrejesha Katalunya winga Mhispania wa Wolves, Adama Traore, ambaye ana umri wa miaka 24, katika dirisha la usajili la majira ya joto. ***(Mail)***

**MARTINEZ AICHAGUA BARCA**

STRAIKA wa Inter Milan na Timu ya Taifa ya Argentina, Lautaro Martinez (22), anajiandaa kukacha ofa za kujiunga na Manchester City na Manchester United katika majira ya joto na badala yake atajipanga kutua Barcelona. ***(Star)***

**LALLANA AGOMBEWA ENGLAND**

KIUNGO wa Liverpool na Timu ya Taifa ya England, Adam Lallana, anatajwa kuwindwa na klabu ya Leicester City. Tottenham, Arsenal na West Ham pia zimeonyesha nia ya kumsajilli nyota huyo mwenye umri wa miaka 31. ***(Telegraph)***

**SPURS, TANGANGA WATETA**

BEKI wa Tottenham, Japhet Tanganga (20), yuko katika mazungumzo ya nyongeza ya mshahara wake ili upandishwe kwa asilimia 1,500% kutoka malipo ya pauni 1,000 kwa wiki anayopokea sasa kutokana na kufanya vizuri tangu alipopandishwa katika kikosi cha kwanza. ***(Mail)***

**ONANA KUMRITHI KEPA**

CHELSEA imeweka wazi nia yake ya kumwania golikipa wa Ajax na Timu ya Taifa ya Cameroon, Andre Onana (23), katika kipindi hiki cha majira ya joto, huku Blues wakijiandaa kuziba nafasi ya Mhispania Kepa Arrizabalaga (25), ambaye yuko mbioni kuondoka klabuni hapo. ***(Goal.com)***

**EVERTON KUTOMUUZA SOARES**

EVERTON haiko tayari kumuuza Everton Soares (23), licha ya mshambuliaji Mbrazil wa Gremio pamoja na Kocha wa Toffees, Carlo Ancelotti na straika Mbrazil Richarlison kuhusishwa na dirisha la usajili litakalofunguliwa na majira ya joto. ***(Liverpool Echo)***

**DAU LA SMALLING HILI**

MANCHESTER United imesema haitakubali kupokea ada ya kiasi cha chini ya pauni milioni 15 ili kumuuza beki wake raia wa England, Chris Smalling, ambaye ana umri wa miaka 30. ***(Team Talk)***

**AWONIYI HAKIJAELEWEKA**

LIVERPOOL imeambiwa inatakiwa kutoa msimamo kuhusu hatima ya straika Mnigeria Taiwo Awoniyi (22), ambaye amekosa namba katika kikosi cha Mainz, tangu alipojiunga na klabu hiyo ya Bundesliga iliyomsajili kwa mkopo wa muda mrefu kwenye kipindi cha majira ya joto mwaka jana. ***(Liverpool Echo)***

**NYOTA LIVERPOOL KUUKATA**

WACHEZAJI wa Liverpool watagawana posho ya pauni milioni nne kama watafanikiwa kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu England msimu huu. ***(Mail)***

HABARI MICHEZO

# MAJIGAMBO YATAWALA AZAM, KMC ZIKIKUTANA

Na Shufaa Lyimo

KOCHA Mkuu wa KMC FC, Haruna Hererimana, amesema kikosi chake kiko tayari kupambana dhidi ya Azam FC katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam.

Hererimana aliliambia gazeti hili kikosi chake kiko vizuri na kila mchezaji amejipanga kuonyesha kiwango cha juu katika mechi ya leo.

Alisema mechi zote za Ligi Kuu Bara zina ushindani, lakini amewataka wachezaji wake kutokuwa na wasiwasi wowote dhidi ya wapinzani wao.

"Nimekiandaa vizuri kikosi changu kwa ajili ya mtanange wa kesho (leo), makosa madogo madogo yaliyokuwapo nimeshyarekebisha, ninaamini watafanya kile nilichowafundisha," alisema Hererimana.

Kocha huyo aliongeza mchezo huo utakuwa mgumu kwa sababu zinaundwa na wachezaji wenye uzoefu na uwezo wa kupambana wakati wote.

"Mchezo wetu utakuwa na ushindani mkubwa, naomba mashabiki wetu waje kwa wingi uwanjani, tunafahamiana vizuri, tumejiandaa kuondoka na pointi tatu," Hererimana aliongeza.

Naye Kocha Msaidizi wa Azam FC, Iddi Cheche, alisema wachezaji wake wako tayari kwa mchezo huo na malengo yao ni kuendeleza kupambana ili kuvuna pointi zote tatu.

"Mechi itakuwa ngumu na yenye ushindani, tunahitaji kuongeza umakini ili kufikia malengo yetu, ligi ni ngumu kwa sababu timu zote zimejiandaa vizuri na zimejipanga kupata matokeo mazuri," Cheche alisema.

Azam FC yenye pointi 38 iko katika nafasi ya pili kwenye msimamo wa ligi wakati KMK walioko katika nafasi ya 15 wana pointi 20 mkononi wakati vinara na mabingwa watetezi wa ligi hiyo ni Simba yenye pointi 50.




Wanariadha wa Kituo cha Mlimani wakiwa katika mazoezi kwa ajili ya kujiandaa na mashindano yatakayofanyika baadaye mwezi huu katika Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam jana. **PICHA : JUMANNE JUMA**

# Polisi Tanzania yafikia malengo

Na Mwandishi Wetu

UONGOZI wa Polisi Tanzania inayoshiriki Ligi Kuu Bara umesema timu yao imetimiza malengo yake iliyojiwekeza katika msimu huu wa mwaka 2019/20 ambao tayari umeingia katika hatua ya lala salama, imeelezwa.

Akizungumza na Nipashe jana, Makamu Mwenyekiti wa Polisi Tanzania, Robert Munisi, alisema timu hiyo iliyopanda daraja msimu huu iliweka malengo ya kumaliza mzunguko wa kwanza wakiwa na pointi 30, ambazo ndio wanazo hadi walipokamilisha hatua hiyo.

Munisi alisema uongozi wa timu hiyo inayotumia Uwanja wa Ushirika mkoani Kilimanjaro inawapongeza wachezaji wake kwa jitihada walizozionyesha licha ya kukumbana na ushindani kutoka kwa timu zote.

"Tuliumia kufungwa na Simba, lakini baada ya kumaliza mechi ile tulifanya sherehe ambayo ilikuwa ni furaha ya kukamilisha mipango yetu, tulidhamiria kumaliza mzunguko wa kwanza na pointi 30, jambo ambalo limetimia, tunaamini mipango haikuwa mibaya kama timu mpya kwenye ligi," alisema Munisi.

Kiongozi huyo aliongeza sasa wameweka mipango ya kukusanya pointi 25 katika mzunguko wa pili na endapo watazikusanya, watakuwa salama.

"Haya ni matunda ya maandalizi mazuri kabla ya msimu, pia tumeongeza wachezaji wapya katika dirisha dogo ambao wataongeza nguvu kwenye kikosi, tunawakumbusha wachezaji wetu kupambana kwa sababu itaisaidia timu kumaliza katika nafasi za juu na vile vile kujitangaza wao binafsi," Munisi alisema.

Alisema kuwa kikosi chao kiliwasili salama jijini Tanga jana mchana kwa ajili ya kuwavaa wenyeji Coastal Union katika mechi ya raundi ya 20 ya Ligi Kuu itakayochezwa kwenye Uwanja wa CCM Mkwakwani.

## Mundu, Uhamiaji kibaruani Unguja

Na Hawa Abdalla, ZANZIBAR

TIMU ya Mundu inatarajia kuvaana na Uhamiaji katika mechi ya kwanza ya mzunguko wa pili wa Ligi Daraja la Kwanza Kanda ya Unguja itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Mau A Kisiwani hapa.

Katibu wa Kamati ya Mashindano ya Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), Hussein Ahmada Vuai, alisema maandalizi ya ligi hiyo yamekamilika na wanazikumbusha klabu zote zinazoshiriki kufuata kanuni.

Vuai alisema mechi za mzunguko wa pili wa ligi hiyo zitachezwa katika viwanja Mjini Unguja na nje kidogo ya mji tofauti na ilivyokuwa kwenye mzunguko wa kwanza.

"Ligi hii itaanza kwa Mundu kuikaribisha Uhamiaji katika uwanja wa Mau A, na mechi nyingine Dulla Boys watavaana na Bweleo kwenye Uwanja wa Bungi na Wachuma Asumini, timu ya Kikwajuni watapepetana na Miembeni katika Uwanja wa Mau B.

Alisema ligi giyo inashirikisha timu 13 ambazo ni Mundu, Uhamiaji, Bweleo, Dulla Boys, Kikwajuni, Taifa Jang'ombe, Kilimani City, Mwembe Makumbi, Miembeni, Ngome, Black Sailor, Idumu na Mchangani United.

## Amri kuibakisha Mbeya City Bara

Na Mwandishi Wetu

TUTABAKI! Hayo ni maneno ya Kocha Mkuu wa Mbeya City, Amri Said, ambaye timu yake inapambana kuhakikisha haishuki daraja kufuatia kufanya vibaya katika mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Akizungumza na gazeti hili jana, Amri alisema wamejipanga kuingia na mbinu tofauti katika hatua hii ya lala salama na anaamini nafasi ya kurekebisha makosa yaliyofanyika katika mzunguko wa kwanza bado ipo.

"Tuko katika wakati mgumu, lakini bado hatujakata tamaa, ni wazi timu yangu inapitia kipindi kigumu kwa sasa kutokana na kushindwa kupata matokeo tuliyotarajia," alisema Amri baada ya kumaliza kucheza dhidi ya KMC.

Kocha huyo alisema wamejipanga kucheza kwa mfumo tofauti na hiyo itakuwa siri pekee ya kuvuna pointi na hatimaye kujiondoa katika mstari wa hatari.

"Tutapambana hadi dakika ya mwisho, mzunguko wa pili ndio umeanza, ninaamini upepo mbaya ambayo Mbeya City ilianza nao msimu huu utageuka, kila mmoja ana kiu ya mafanikio kwenye kikosi hichi," Amri aliongeza. Katika msimamo wa Ligi Kuu Bara, Mbeya City ipo kwenye nafasi ya 18 ikiwa na pointi 14 mkononi.

# Michezo

Jumamosi Februari 8, 2020

Nipashe




Ronaldo afunguka angekuwa mvuvi HABARI UK 30



Kiungo wa Simba, Ibrahim Ajib (kushoto), akiwania mpira dhidi ya beki wa JKT Tanzania, Edward Songo, katika mechi ya Ligi Kuu Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam jana. Simba ililala bao 1-0. **PICHA : JUMANNE JUMA**

# JKT TANZANIA YAIZIMA SIMBA

## ●●●Yapoteza mchezo wa pili katika Ligi Kuu Bara msimu huu, lakini ikiendelea kuongoza katika msimamo...

**Na Adam Fungamwango**

MABINGWA watetezi, Simba wamepoteza mechi ya pili msimu huu baada ya kukubali kichapo cha bao 1-0 kutoka kwa 'Maafande' wa JKT Tanzania katika mchezo wa Ligi Kuu Bara uliochezwa kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam jana.

Mara ya mwisho Simba kupoteza mechi ya Ligi Kuu Bara ilikuwa ni Oktoba 30, mwaka jana kwenye Uwanja wa Kambarage mjini Shinyanga ilipochapwa bao 1-0 dhidi ya Mwadui FC.

Alikuwa ni Adam Adam, mchezaji wa zamani wa African Lyon na Prisons ya Mbeya aliyepeleka kilio Msimbazi kwa kufunga bao pekee katika mchezo huo.

Straika huyo tegemeo ambaye amefikisha magoli matano mpaka sasa, alifunga bao hilo dakika ya 24 kwa kichwa baada ya mabeki wa Simba kushindwa kuokoa mpira wa krosi ulipigwa kutoka winga ya kulia, mfungaji akiruka bila bugudha na kuujaza wavuni.

Dakika ya kwanza tu, JKT Tanzania walikosa bao la wazi baada ya mabeki wa Simba kuzembea kuuokoa mpira wa kurushwa ambao ulimkuta Daniel Lyanga akiwa yeye na kipa, Benno Kakolanya lakini alipiga shuti fyongo lililotoka nje.

Shambulio pekee la maana kwa Simba lilikuwa dakika ya 44 baada ya kipa wa JKT Tanzania, Patrick Muntari kushindwa kupiga mpira mbele, badala yake ulifika miguuni mwa Ibrahim Ajibu ambaye alipiga shuti hafifu lilioishia tena miguuni mwa kipa huyo.

Kipindi cha pili Simba ilifanya mabadiliko kwa kuwatoa Shiza Kichuya, Gerson Fraga na Ajibu, na nafasi zao zikachukuliwa na Nahodha John Bocco, Francis Kahata na Claotus Chama ambao walileta uhai, lakini mabeki wa JKT Tanzania wakiongozwa na Michael Aidan walikaa imara kuokoa hatari zote.

Simba watajutia nafasi mbili za wazi walizozikosa dakika ya 59, Luis Miquissone akicheza mechi yake ya kwanza kwenye klabu hiyo, alipopiga shuti lililopaa juu kidogo ya lango baada ya kupata pasi kutoka kwa Kahata na nyingine ilikuwa dakika ya 89, Medie Kagere alipoukosa mpira wa krosi kutoka kwa Chama. Baada ya mechi hiyo kumalizika, Bocco alisema walipambana kwa kiasi cha kutosha, lakini bahati haikuwa yao.

"Tumepambana, lakini bahati haikuwa yetu, ila niwapongeza JKT Tanzania kwa sababu walikuja na 'plani' yao ambayo wameifanikisha. Ila tumamaliza mechi hii, akili yetu iko kwenye mechi inayofuata kwa sababu tayari tumeshapoteza," alisema nahodha huyo.

Kwa matokeo hayo Simba inasalia na pointi zake 50 ikiwa imecheza mechi 20, huku JKT Tanzania ikifikisha pointi 30 kwa mechi 20 ambazo imecheza na kukamata nafasi ya nane kwenye msimamo wa Ligi Kuu Bara.

Ligi hiyo itaendelea tena leo kwa Ruvu Shooting kuivaa Yanga, KMC kucheza dhidi ya Azam FC, Coastal Union kuwakaribisha Polisi Tanzania, Alliance watachuana na Mbao, Ndanda watawakabili Namungo, Singida United dhidi ya Mwadui FC, Prisons wao watawaalika Mbeya City, Mtibwa Sugar watacheza na Lipuli huku Biashara United wakiwafuata Kagera Sugar.

# Yanga, Ruvu ngoma nzito

**Na Somoe Ng'itu**

IKIWA na kumbukumbu ya kufungwa katika mechi ya fungua pazia msimu huu, Yanga imejipanga kulipiza kisasi itakapoivaa Ruvu Shooting katika mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara utakaochezwa leo kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam.

Yanga ikiwa mwenyeji katika mchezo wa raundi ya kwanza, ilikubali kichapo cha bao 1-0, kutoka kwa 'Maafande' hao wa Mlandizi, Pwani.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Yanga, Luc Eymael, amesema wachezaji wake wapo tayari na kamili kwa ajili ya mechi hiyo na anaamini watafanya vizuri.

Eymael alisema wamejipanga kuendeleza kasi ya ushindi na kila mchezaji amempa jukumu lake ili kuhakikisha wanapata matokeo mazuri katika mechi hiyo.

"Tunataka kuanza mzunguko wa pili vizuri, wachezaji wanaonyesha ari na nia ya kupambana kwa ajili ya timu, ligi ina ushindani mkubwa na kila timu inahitaji matokeo, hata sisi pia tunahitaji ushindi, katika mechi hiyo," alisema Eymael.

Naye Ofisa Habari wa Yanga, Hassan Bumbuli, aliliambia gazeti hili Ruvu Shooting wasitarajie kuokota 'dodo' chini ya mbuyu katika mechi ya leo kama ilivyokuwa kwenye mchezo wa kwanza wa ligi hiyo.

"Ushindi wao ulikuwa wa kubahatisha, kikosi kile kilikuwa chini ya Zahera (Mwinyi), sasa hivi kuna 'silaha' mpya ambazo pia ziko chini ya mwalimu mpya, wasitarajie tena kuokota dodo chini ya Mbuyu, hilo halipo kwa sasa tuna mpango mwingine kabisa," alisema Bumbuli.

Alisema kikosi chao kimeimarika na kimejipanga kuanza duru ya pili kwa ushindi na kuendelea na mbio za kuwania ubingwa.

Masau Bwire, Ofisa Habari wa Ruvu Shooting, alisema timu yake inahitaji kuendeleza 'ubabe' dhidi ya Yanga na wanatarajia wanapata ushindi mnono kutokana na wachezaji wao walivyoimarika.

"Kikosi chetu kiko imara na tumejiandaa kukutana na Yanga, ni ile ile ila ina mabadiliko ya wachezaji wachache, tunaendelea na kampeni yetu ya kupapasa kama ilivyo ada. Ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Mtibwa Sugar, umetupa ushindi mdogo, tunapenda kushinda mabao zaidi ya mawili," Bwire alitamba.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >